**WARUNDI** wanaodaiwa kuuza alkasusu Dar kortini madai uhamiaji

UKURASA 3



**IGP** Sirro aona dawa kuukabili ujambazi nchini

UKURASA 4


ama
AFYA NA MAZINGIRA
MABADILIKO SEKTA YA MAJI: NYASA WAJIBIWA
Mradi 'Safari City' utakavyong'arisha upya mazingira ya jiji la Arusha
Lilivyokuwa baa la volkano, wenyeji kutawanyika mbio DRC hadi Rwanda

UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Mei 27, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580593

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710


## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

**MTOTO AKUTWA AMEJINYONGA CHOONI NYUMBANI**

MWANAFUNZI Najima Said (14) anayesoma darasa la saba katika Shule ya Msingi Mtongani Wilaya...

**UKURASA WA 3**

**MWINYI ATAJA SIRI KUTUMIA KISWAHILI**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, anasema ameamua...

**UKURASA WA 7**

**MASHINE ILIYOZAMA BANDARINI YAOPOLEWA**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari (TPA) imefanikiwa kuiopoa mashine...

**MADALALI KUBANWA KULIPA KODI**

UKURASA 5


# Mbowe: Hatutashiriki Uchaguzi Mkuu 2025

**ATAJA** masharti yao, awasiliana na Samia...*Endelea Uk. 2*



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe, akizungumza na viongozi wa wilaya sita za mkoa wa Arusha jana, kuhusu mikakati ya ujenzi wa chama sambamba na uzinduzi wa mpango wa usajili wa wanachama kwa njia ya kielektroniki. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Serikali kuruhusu kilimo cha bangi



UKURASA 2


**MICHEZO** **YANGA YAJIGAMBA KITAELEWEKA** UK. 24

**MAONI, KATUNI UK. 6**

# Mtoto akutwa amejinyonga chooni nyumbani kwao

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MWANAFUNZI Najima Said (14) anayesoma darasa la saba katika Shule ya Msingi Mtongani Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani, amekutwa amejinyonga ndani ya choo nyumbani kwao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, amethibisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kwamba lilitokea Mei 22, mwaka huu.

Kamanda Wankyo alisema upelelezi umebaini kuwa chanzo cha kifo cha mtoto huyo ni kutuhumiwa na mama yake kuiba Sh. 5,000 nyumbani.

Alisema Jeshi la Polisi linamshikilia mama wa marehemu, Ashura Selemani na baba mlezi kwa mahojiano zaidi.

Katika tukio lingine, Kamanda Wankyo alisema mtu mmoja aliyejulikana kwa jina la Mrisho Omary alifariki dunia baada ya nyumba waliyokuwa wamelala kuchomwa moto.

Alisema katika tukio hilo ambalo lilitokea hivi karibuni eneo la Umwelani Kata ya Kongowe, watu watatu wakiwa wamelala kwenye nyumba iliyoezekwa kwa udongo ilichomwa moto na watu ambao hawajafahamika.

Alisema watu waliokuwa wamelala katika nyumba hiyo ni Mrisho Omari, Mwalimu Ally na Lusekelo ambao walichomewa nyumba wakituhumiwa kuwa ni wezi.

Kamanda Wankyo alisema Mrisho alifariki dunia kutokana na majeraha ya moto, huku wengine wawili wakiwa wamelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Tumbi wakiendelea na matibabu.

Kamanda Wankyo alisema: "Upelelezi wa awali umebaini kuwa kulikuwa na ugomvi wa kimapenzi baina ya Zuwena Mahira na watu hao."

Alisema upelelezi wa tukio hilo unaendelea kuwabaini waliohusika na tukio la kuchoma moto nyumba hiyo.

# Mbowe: Hatutashiriki uchaguzi 2025

**Na Waandishi Wetu,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema chama hicho hakitashiriki Uchaguzi Mkuu ujao kama mchakato wa Katiba Mpya utaendelea kuwekwa kapuni.

Mbowe alitoa msimamo huo jana jijini, akisisitiza kwamba wanakusudia kupita nchi nzima kuidai katiba hiyo kwa kuwa ni haki ya wananchi.

Alikuwa akizindua mfumo wa kielekroniki wa chama hicho wa kuwatambua wanachama wake.

"Tunaposema tunahitaji Katiba Mpya, tutawafundisha wanachama na viongozi wetu, watambue umuhimu na uzito wake, kwa sababu udhaifu wa katiba yetu ya sasa umesababisha kuwa na kiongozi aliyekuwa madarakani kuharibu nchi, kuumiza na kuwatesa wananchi kwa kuwa katiba hii inampa mamlaka makubwa ya kifalme.

"Rais akisema mfunge mtu huyu, sitaki kuona mikutano ya hadhara au kuona kiongozi wa upinzani, anashinda uchaguzi na haki za wananchi wote milioni 60 zinapotea shauri ya kiongozi mmoja mwenye madaraka na mamlaka makubwa kutokana na udhaifu wa katiba hii ya sasa," alifafanua.

Mbowe alisema tayari ameshazungumza na Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu suala la Katiba Mpya, kwamba siyo mapenzi ya mtu mmoja, bali ni mapenzi ya taifa.

"Nimemwambia Mama Samia (Rais), mambo ya katiba siyo mambo ya mapenzi yake, ni mapenzi ya taifa la Tanzania na Katiba Mpya tutaitafuta na kuipigania kwa jasho na damu ili kupata katiba ya nchi yetu kabla ya uchaguzi wa mwaka 2025," alisema.

Katika hatua nyingine, Mbowe, alimpongeza Rais Samia kwa kile ambacho alikiita kurudisha tabasamu na matumaini kwa wananchi akidai walipoteza imani na viongozi kutokana na baadhi ya mambo maovu.

"Mama (Rais) amerejesha matumaini na tabasamu kwenye sura za Watanzania na CHADEMA, kwa hilo tunamuunga mkono na nilimwandikia ujumbe wa kutaka kuonana naye kwa ajili ya mazungumzo.

"Alinijibu kwamba tutakutana na kuzungumza, hivyo basi tunasubiri nafasi hiyo ya mazungumzo kwa kuwa kuna mambo mengi mabaya yamefanyika kwenye nchi hii," alisema.

Mbowe alidai kuwa moja ya mambo watakayoyawasilisha kwa Mkuu wa Nchi ni kitendo cha wafuasi wa chama hicho zaidi ya 250 kufungwa gerezani huku akidai baadhi yao wameshtakiwa kwa makosa ya kubambikwa ukiwamo unyang'anyi, uhujumu uchumi, mauaji na ubakaji.

Pia alitangaza mkakati wa CHADEMA kuanza kujenga ofisi za chama hicho kuanzia ngazi ya wilaya, mikoa na kanda ili kuongeza imani kwa wanachama wake, kuwaziba midomo baadhi ya makada kutoka vyama vingine vya siasa kuwa chama hicho hakina ofisi.

Alisema kuwa baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana, walipaswa kupokea ruzuku ya Sh. milioni 140 kwa mwezi, lakini waliikataa kutokana na kutoutambua uchaguzi huo.

"Atakayeomba kurudi na kuomba msamaha tumpokee na kumsamehe kwa kuwa chama chetu hakihukumu bali tunataka kujenga taifa lenye haki na mshikamano pasipo kuwabagua watu kutokana na itikadi za vyama, sura, rangi, kabila au dini," alisema.

●**Imeandikwa na Allan Isack na Cynthia Mwilolezi**



Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Gerald Kusaya, akifungua kikao kazi kati ya mamlaka hiyo na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali kuruhusu kilimo cha bangi

**Na Waandishi Wetu**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imesema imefanya marekebisho ya kifungu cha 12 ili kuruhusu kilimo cha bangi kwa ajili ya tiba na utafiti.

Kaimu Kamishna wa Kitengo cha Huduma za Sheria, Christina Rwehabuza, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mafunzo ya mpango kazi kwa ajili ya kutambua mchango wa waandishi wa habari katika kutoa elimu kwa jamii kuhusu dawa za kulevya.

Katika mafunzo hayo, Rwehabuza alisema kila wakati amekuwa akiulizwa maswali kuhusu kifungu cha 12 kama mamlaka imeshatengeneza kanuni za kuruhusu ulimaji wa bangi.

"Kifungu hicho ndiyo kimerekebishwa, kwa hiyo kanuni kuhusu kuruhusu bado hatujazitengeneza kwa sababu Umoja wa Mataifa (UN) wanaendelea kulifanyia kazi suala hilo waje watoe tamko ili nchi zote zitengenezewe miongozo," alisema.

Alisema hata ikitokea wataruhusu ulimaji wa bangi, haitalimwa kiholela lazima wajiridhishe na kilimo hicho kitakuwa ni kwa ajili ya tiba na utafiti. Akizungumzia sheria mwaka 2015 kama ilivyorekebishwa mwaka 2019 alisema imegawanyika sehemu saba na sehemu ya pili inazungumzia makatazo ya kujihusisha na dawa za kulevya.

Alitolea mfano endapo mmiliki wa ardhi akamkodisha mtu alime halafu akalima bangi, ikithibitika mmiliki atafungwa kifungo cha miaka mitano na kisichozidi miaka 30 na fani isiyopungua milioni tano au isiyozidi milioni 50.

Rwehabura alisema sheria ya dawa za kulevya inaelekeza utoaji wa adhabu ikiwamo kutumia, kuwezesha, kusafirisha na kumpangisha nyumba muuza dawa za kulevya.

"Ukikutwa na mitambo ya kutengeneza dawa za kulevya, adhabu yake ni jela maisha na faini ya Sh. milioni 200, kwa watumiaji faini yake ni isiyopungua Sh. milioni moja au jela miaka mitatu," alisema.

Alisema kumpangisha muuzaji wa dawa za kulevya kwenye nyumba faini ni isiyopungua Sh. milioni tano, jela miaka mitano au isiyozidi miaka 30 au adhabu zote kwenda sambamba.

Alisema kwa wale wanaofadhili watu kufanya biashara hiyo adhabu ni jela maisha na faini ya Sh. bilioni moja.

Kamishna Jenerali wa DCEA, Gerald Kusaya, alitaka wananchi na waandishi wa habari wawe na imani na mamlaka kwa sababu wana watumishi ambao wanawafuatilia siku hadi siku hivyo hakuna taarifa ya siri itakayotoka nje.

"Mapambano tumeyapa sura mpya, wote wanaojihusisha au kuwa na wazo la kutaka kujihusisha na dawa za kulevya ni vyema watafute biashara nyingine kwa sababu tunafanya kazi usiku na mchana kama ni kupumzika ni baada ya kufa, tunataka kizazi kisichotumia dawa za kulevya," alisema.

Alisema waandishi wa habari wana nafasi kubwa kuieleza jamii dawa za kulevya zinapaswa kuchukiwa kwamba zinapotosha nguvukazi ya taifa.

Kamishna wa Kinga na Tiba wa Mamlaka hiyo, Dk. Peter Mfisi, alisema mtumiaji wa dawa za kulevya yeyote mara anapotumia inaharibu mfumo wa fahamu wa binadamu na kwamba si kitu cha kufanyia mzaha.

**Imeandaliwa na Romana Mallya na Hellen Mwango**



Raia wa Burundi 29, wakiwa katika chumba cha Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, kabla ya kusomewa mashtaka ya uhamiaji haramu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Raia wa Burundi kortini tuhuma uhamiaji haramu

**Na Kulwa Mzee**

RAIA 29 wa Burundi wanaodaiwa kuuza kahawa aina ya alkasusu na kahawa ya kawaida, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakituhumiwa kuingia nchini na kuishi kinyume cha sheria.

Kati yao, washtakiwa 13 wamekiri makosa wakiwamo watoto wanne na wengine 16 wamekana mashtaka hayo.

Washtakiwa walisomewa mashtaka yanayomkabili mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, jana.

Wakili wa Serikali, Godfrey Ngwijo, aliwataja washtakiwa hao kuwa ni pamoja na Kassim Mkoko, Elias Shadra, Hilary Lozo, Richard Dismas, Ntahondereye Reverie, Baraka Yosam, Meraki Noah, Robert Lazaro, Samson Erick, Kazimana Aimable, John Ayoub, Donald Kasendi, Elias Jonias, Shabani Makangila, Minani Festo, William Aston, Salasio Jeradi, Niubuntu Baraka, Majaliwa Novatus, Nionkuru Odasi, Boniface Chubwa.

Wengine ni Shabani Mussa, Jedio Misigo, Kuruwa Cpliano, Shadrack Bagoye, Daud Yokonia, Steven Mkonu, Asheri Selekela na Mussa John.

Washtakiwa ambao ni watoto chini ya miaka 18, wamewekwa chini ya Ustawi wa Jamii.

Mahakamani huko washtakiwa wote walisomewa mashtaka mawili ya kuingia nchini bila viza na lingine la kuishi nchini bila viza.

Wakili Godfrey alidai washtakiwa walitenda makosa hayo Mei 25, mwaka huu, maeneo mbalimbali ya Kariakoo na Jangwani.

Wakili wa Serikali, Godfrey, aliomba mahakama iahirishe kesi ili ipangwe tarehe nyingine kwa ajili ya kuwasomea washtakiwa maelezo ya awali.

Hakimu Shaidi alikubali kuahirisha kesi hiyo hadi Juni Mosi mwaka huu kwa ajili ya kuwasomea washtakiwa waliokiri na kuwapa muda washtakiwa waliokana, kutafakari na kufika na vibali vilivyowaruhusu kuishi nchini.

Kesi itakuja Juni Mosi mwaka huu na washtakiwa wote walipelekwa mahabusu isipokuwa watoto ambao walikabidhiwa kwa Idara ya Ustawi wa Jamii hadi tarehe ya kesi ijayo.

# Kifusi chaua wachimbaji

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

WATU wawili wamekufa baada ya kufukiwa na kifusi cha udongo walipokuwa wakichimba madini katika Kitongoji cha Maponda,Kijiji cha Igurubi, wilayani Igunga, mkoani Tabora.

Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kata ya Igurubi, Godfrey David, aliwataja waliokufa ni Mrisho Luge (32), mkazi wa Arusha na Mussa Cosmasi (41), mkazi wa Masumbwe, mkoani Geita.

David alifafanua kwamba tukio hilo lilitokea juzi usiku wakati wachimbaji hao wakiwa katika mgodi namba tano wakichimba madini na ndipo ghafla waliangukiwa na ukuta wa udongo na kisha kufariki dunia papo hapo.

Kwa mujibu wa Mtendaji huyo, baada ya kupata taarifa hiyo ndipo yeye kwa kushirikiana na wanachi walifanya jitihada za kuitoa miili ya watu hao katika shimo hilo na kukuta watu hao wameshakufa.

Naye Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Sofia Jongo, alithibitisha kufariki kwa watu hao na kwamba chanzo cha vifo hivyo ni kufukiwa na ukuta wa udongo.

# Mwinyi ataja siri kutumia Kiswahili kuandika kitabu

**Na Christina Mwakangale**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, anasema ameamua kuwaheshimisha Watanzania kwa kutumia lugha ya Kiswahili katika uandishi wa kitabu chake.

Katika kitabu hicho alichokiita 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', Mwinyi anasema anakumbuka heshima aliyopewa na Watanzania ambayo haikuishia katika kuwaongoza bali kumtambua kama bingwa wa Kiswahili.

Anasema amekuwa akihimiza matumizi sahihi ya lugha hiyo, akiitaja kama silaha ya kuimarisha utambuzi na umoja wa Watanzania.

"Kabla ya kuanza kuandika tawasifu hii, nilijishauri sana iwapo niiandike kwa Kiingereza au kwa Kiswahili.

"Lakini nikakumbuka heshima ambayo Watanzania wenzangu walinipa, si kuwa rais wao tu bali kunitambua kama mmojawapo wa mabingwa wa Kiswahili," anasema.

Anakumbusha Januari 23 mwaka 1955 Baraza la Kiswahili (BAKITA) liliamua kumkabidhi tuzo kubwa ya kutambua mchango wake katika lugha hiyo, akivishwa nishani ya Shaaban Robert.

"Niliwahi kuwa Mwenyekiti wa BAKITA kwa karibu miaka 10, kuanzia mwaka 1968 hadi 1977, hadi nilipoteuliwa kuwa Balozi wa Tanzania Misri, ikabidi niondoke.

"Wa kupewa sifa kubwa na shukurani kwa kutufikisha hapa hadi tukawa lugha ya jumuiya ni Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kabla ya uhuru aliweka wazi kuwa lazima tuimarishe Kiswahili, lugha ya taifa," anasifu.

Mzee Mwinyi anakitaja Kiswahili kama sumaku kwa kuwa kinawavuta wanaokiongea kuwa karibu wao kwa wao na kwamba kimeenea nchi nyingi na kuvuta mapenzi ya wengi hadi kuwa miongoni mwa lugha rasmi za Umoja wa Afrika (AU).

Mwinyi anasema bado ushauri wa Mwalimu Nyerere kuhusu lugha hiyo, kwamba wakati Kiswahili kikiendelea kukuzwa, Kiingereza kisipuuzwe kwa kuwa ni lugha ya kimataifa.





Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, akionyesha silaha aina gobore kwa waandishi wa habari jana, iliyotumika kwenye tukio la mauaji ya raia mmoja anayesadikiwa ni mwizi wa mifugo, katika kijiji cha Nhinhi, wilayani Chamwino, mkoani humo. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# IGP Sirro aona dawa kuukabili ujambazi nchini

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, amewaagiza wamiliki wa kampuni za ulinzi binafsi kuacha kuajiri walinzi wazee na kuhakikisha wanapowapeleka kwenye malindo wawe na silaha mbili ili moja ilinde nyingine.

IGP Sirro alitoa maagizo hayo juzi jioni baada ya kufanya ziara katika kituo cha mafuta cha MEXONS Bunju kilichoko Mwabepande jijini Dar es Salaam ambacho Mei 7, mwaka huu, kilivamiwa na watu wanaodaiwa kuwa ni majambazi na kupora silaha aina ya shot gun na Sh. milioni 2.4.

Ziara hiyo pia ilihusisha duka la mfanyabiashara wa jumla lililoko Mabibo ambaye amenusurika kifo, baada ya kujeruhiwa kwa kupigwa risasi na watu wanaodhaniwa majambazi ambao hawakufanikiwa kupora chochote.

Akizungumza baada ya ziara hiyo, IGP Sirro alisema amebaini uzembe wa kampuni ya ulinzi inayolinda kituo cha mafuta kilichovamiwa kwa sababu kimeweka mlinzi mmoja mwenye silaha na mwingine akiwa hana hivyo kutoa mwanya kwa wahalifu.

Alisema kituo hicho kipo eneo la porini na mlinzi anayelinda ni mzee na mwenye silaha ni mmoja.

"Ninalipongeza Jeshi la Polisi mkoa wa Kinondoni wameweza kuwakamata wote pamoja na silaha iliyonyang'anywa siku ya tukio. Mmoja alikimbia lakini bado anaendelea kufuatiliwa," alisema.

IGP Sirro alitoa wito kwa kampuni za ulinzi kuwa haikubaliki mlinzi kwenye eneo la lindo mmoja ndiyo awe na silaha na mwingine hana.

"Siku zote silaha moja inalindwa na nyingine kwa hiyo maelekezo ninayotoa kwa kampuni mahali kwenye silaha hakikisha zinakuwapo mbili kwa maana kwamba walinzi lazima wasaidiane, jambazi mmoja akimnyang'anya mlinzi mmoja silaha, nyingine inasaidia kumwokoa mwenzake," alisema.

IGP Sirro aliwataka wanaojenga kisima cha mafuta maeneo ya pembezoni wawe na mawasiliano na Jeshi la Polisi mara kwa mara wapite doria kwa sababu kuamini walinzi tu siyo sawasawa kwa kuwa askari polisi wanakuwa na silaha kubwa yenye uwezo.

"Nimekuja Dar es Salaam ili kupita katika kampuni za ulinzi, wazee wameshastaafu afanye kazi za uzee nyumbani siyo kuingia kwenye malindo wakati nguvu hakuna, umeshafikisha miaka 60 pumzika, isijekufa kwenye malindo bila sababu, wakurugenzi wote wa kampuni za ulinzi binafsi, vijana wenye umri mdogo na nguvu kuanzia miaka 18 hadi 50 na wapo wengi waajiriwe," alisema.

Pia alizitaka kampuni hizo kuacha ubahili na kutafuta walinzi wa bei nafuu.


**TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC**

**Mwenyekiti na Wanahisa,**

**Yah: Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa**

Taarifa inatolewa kwamba **Mkutano Mkuu wa Saba wa Wanahisa wa Tandahimba Community Bank** utafanyika siku ya **Jumamosi tarehe 19 Juni, 2021,** katika **Maghala ya Chama cha Ushirika TANECU,** Tandahimba kuanzia saa tatu kamili **(Saa 3.00)** asubuhi kujadili dondoo zifuatazo:

1. **Kufungua Mkutano.**
2. **Kuridhia Dondoo.**
3. **Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu uliopita.**
4. **Kujadili yatokanayo na Mkutano Mkuu uliopita.**
5. **Kujadili na kupokea Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za mwaka 2020.**
   - 5.1 Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi.
   - 5.2 Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2020.
6. **Taarifa kuhusu Mtaji wa Benki.**
7. **Kuidhinisha Uteuzi wa Mkurugenzi wa Bodi.**
8. **Kuidhinisha Ada ya Wakurugenzi.**
9. **Kuteua Wakaguzi wa Hesabu.**
10. **Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.**
11. **Kupanga mahali na tarehe ya Mkutano ujao.**
12. **Kufunga Mkutano.**

**Maelezo:**

1. *Daftari la Wanahisa litafungwa tarehe 18/06/2021 na litafunguliwa tena tarehe 21/06/2021.*
2. *Makabrasha ya Mkutano yatapatikana katika Makao Makuu ya Benki kuanzia tarehe 07/06/2021 na kwenye Ukumbi wa Mkutano tarehe 19/06/2021.*
3. *Wanahisa wana haki ya kutuma wawakilishi kwa kuwapa hati ya hisa na fomu ya uwakilishi iliyojazwa kikamilifu.*
4. *Wanahisa watakao hudhuria Mkutano watajigharamia usafiri na malazi.*

**Kwa mawasiliano tafadhali tumia anuani ifuatayo:**
**Katibu wa Benki,**
**Tandahimba Community Bank Plc,**
**S. L. P. 06, Tandahimba. MTWARA.**

**KWA IDHINI YA BODI**

**J. B. Rugambo**
**KATIBU**
**20 Mei, 2021**


# Waziri: Ulinzi umeimarishwa mpakani na Msumbiji

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, amesema ulinzi na usalama umeimarishwa katika mipaka yote katika kudhibiti mapigano yanayoendelea Kaskazini mwa Msumbiji, Kusini mwa Tanzania katika Jimbo la Cabo Delgado.

Amesema majeshi ya nchi yapo kazini kuhakikisha wanalinda mipaka na wakimbizi wanaotoka Msumbiji kuja Tanzania kuhakikisha wanatolewa mipakani na kurudishwa katika miji ya katikati ya nchi ya Msumbiji.

Balozi Mulamula aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika mkutano wa mabalozi wanaowakilisha nchi mbalimbali, wawakilishi wa Umoja wa Mataifa, wataalamu mbalimbali wakiwamo mabalozi wastaafu.

Mkutano huo uliandaliwa na Kituo cha Sera za Kimataifa (CIP), kwa lengo la kuangalia hali ya usalama Msumbuji kutokana na sintofahamu iliyoibuliwa na vikundi vya waasi.

Alisema wanajeshi wa Tanzania wanashirikiana na wa upande wa pili wa Msumbiji pamoja na viongozi wa mikoa wenye jukumu la kusimamia ulinzi na usalama katika maeneo husika.

"Kuhusu wakimbizi wanaokuja upande wetu hatuwarudishi bali tunawachukua na kuwapeleka mahali salama, hatuwezi kuweka kambi ya wakambizi sehemu ambayo ipo wazi katika nchi yetu, vikundi vya ugaidi vitaweza kuhamia katika maeneo ya nchi yetu," alisema na kuongeza kuwa:

"Sisi kazi yetu ni kuwalinda na kutoa ushirikiano wa kuwatoa wakimbizi katika maeneo ya mipaka yetu wasiwe mpakani au karibu na mipaka ambayo magaidi ndiyo walipo bali tunawachukua na kuwarudisha katika maeneo ya katikati ya Msumbiji.

Balozi Mulamula alisema tangu mashambulizi yameanza nchi za SADC na viongozi wa nchi hizo wamekuwa wakikutana katika kutafuta suluhu ya kuleta amani na usalama endelevu katika eneo hilo.

Alisema kupitia mkutano huo wadau hao wapanue wigo wa kuangalia hali ya Msumbiji katika masuala mtambuka ambayo yanasababisha ukosekanaji wa amani au yanaleta amani.

"Katika mambo hayo angalieni suala la maendeleo, kwa sababu umaskini ukizidi vikundi hivi vya waasi vinatumia kama upenyo wa kuwatumia vijana wetu ambao waliokata tamaa na maisha," alisema na kuongeza:

Mwenyekiti wa CIP, Profesa Rwekiza Mulandara, alisema katika majadiliano hayo wataangalia suala la kutafuta suluhu ya mgogoro huo.

## HABARI KITAIFA

# Serikali kuwabana madalali kulipa kodi

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imekuja na vipaumbele sita kwa mwaka wa fedha 2021/22 ikiwa ni pamoja kutambua, kupima na kumilikisha vipande vya ardhi zaidi ya milioni 2.5 mijini na hati za kimila milioni 2.6 vijijini.

Vilevile, imesema inakuja na mwongozo kwa madalali ili walipe kodi na kufanya kazi kwa uhalali ili kutowaumiza wananchi, kuongeza kasi ya upimaji ardhi na utatuzi wa migogoro ya ardhi.

Akiwasilisha bungeni jana makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha Waziri Willium Lukuvi alivitaja vipaumbele vingine kuwa ni kuandaa mipango kabambe ya matumizi ya ardhi, kuendeleza miji, maeneo tengefu, visiwa, ukanda wa pwani na kutenga ardhi ya kutosha (hazina ya ardhi) kwa ajili ya uwekezaji, kuimarisha uwekezaji katika ujenzi wa nyumba za gharama nafuu.

Pia kuboresha mfumo wa usimamizi wa taarifa za ardhi kwa kutumia TEHAMA, kuwianisha mifumo ya usimamizi wa ardhi na mipango ya maendeleo ya sekta zingine katika matumizi ya ardhi na kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika upimaji wa ardhi.

Waziri Lukuvi alisema ardhi ni rasilimali kuu kwa jamii na matumizi yake ni mtambuka, hivyo maendeleo katika sekta mbalimbali nchini yanategemea ardhi.

Alisema wizara itaendelea kutambua, kupanga, kupima na kumilikisha ardhi, hatua ambayo ni suluhisho la kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi.

Kwa mujibu wa Lukuvi, serikali itaendelea kutambua na kuhakiki uwekezaji katika ardhi ili kutambua mchango wake katika uchumi wa nchi.

Alifafanua katika muda wa kati wa miaka mitano Wizara inalenga kupima takribani asilimia 37 ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji, makazi, biashara na matumizi mengine ya ardhi.

"Lengo hilo litafikiwa kwa kutekeleza miradi mbalimbali katika mamlaka za upangaji kwa kushirikiana na mamlaka za serikali za mitaa na wadau wengine chini ya uratibu wa wizara," alisema.

**DENI BILIONI 82/-**

Waziri huyo pia alisema deni la taasisi za umma kwa kodi ya pango la ardhi limefikia Sh. bilioni 82 na kwamba jitihada zinaendelea na kuwataka wananchi ambao ardhi imetambuliwa, imepimwa au kumilikishwa, kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati ili kuepuka tozo ya adhabu au kuchukuliwa hatua za kisheria.

Waziri huyo alisema katika mwaka wa fedha 2021/22, wizara imepanga kukusanya Sh. bilioni 260 kutokana na kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali zinazohusiana na Sekta ya Ardhi.

# Wawili mbaroni kwa tuhuma za mauaji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Dodoma, linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za mauaji ya mkazi wa Kijiji cha Nhinhi kilichopo wilayani Chamwino, Samson Kikoti (56), kwa madai kuwa ni mwizi wa mifugo.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Gilles Muroto, aliwataja watuhumiwa ni Simon Kikoti (36) na George Mhando.

Alisema Samson aliuawa Mei 23, mwaka huu, majira ya saa 1:20 usiku. Alisema baada ya mauaji hayo, ulifanyika msako na kuwakamata watuhumiwa hao na kukutwa na silaha mbili aina ya gobole zilizotumika katika mauaji hayo.

"Baada ya kuhojiwa watuhumiwa wamekiri kuhusika na mauaji hayo kwa kutumia silaha na chanzo ni kujichukulia sheria mkononi kwa kumtuhumu marehemu kuwa ni mwizi wa mifugo wa muda mrefu, watuhumiwa watafikishwa mahakamani kwa kosa la mauaji," alisema Muroto.

Muroto alisema katika tukio lingine, Jeshi la Polisi limewakamata watu 49 kwa makosa mbalimbali ikiwamo unyang'anyi kwa kutumia bodaboda, dawa za kulevya na wizi wa kuvunja nyumba.

Alisema watuhumiwa walikamatwa katika doria mbalimbali zilizofanywa na jeshi hilo, kwamba kati yao 23 walikamatwa wakicheza kamali kinyume cha sheria.

Pia, alisema watuhumiwa saba walikamatwa kwa matukio ya wizi wa kutumia bodaboda.

Kuhusu dawa za kulevya, Muroto alisema wamemkamata Weston Maula (28) mkazi wa Kiwanja cha Ndege akiwa na bangi gramu 2.8 amefungwa kwenye mfuko wa plastiki na kuficha kwenye koti, huku Juma Shaban (25) na Mrisho Yahya wakikamatwa na misokoto sita ya Bhangi.

Alisema walimkamata, Meck Edward akiwa na bangi zaidi ya gramu 15 akiwa amefunga katika mfuko na Mwita William (63) akiwa na pombe haramu aina ya gongo lita 35.

Alisema pia walifanikiwa kuwakamata watu watano katika eneo la Mwitikila wilayani Bahi wakiwa na mali za wizi.

# Wataja mwarobaini bajeti finyu ya Afya

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Dini Mbalimbali la Amani Tanzania (IRCPT) limeishauri serikali kuweka utaratibu wa kutenga kiwango fulani cha mapato ya kila mwaka na kukielekeza kwenye mfuko maalum wa afya.

Kwa mujibu wa baraza hilo, utaratibu huo utaboresha huduma za afya badala ya kutegemea bajeti ya serikali katika wizara husika ambayo mara nyingi haitolewi kama ilivyoidhinishwa na Bunge.

Mratibu wa Kamati ya Viongozi wa Dini Mbalimbali, Edmund Matotay, alisema jijini Dar es Salaam jana kuwa suala la afya ni nyeti, hivyo huduma ya lazima kwa wananchi wote na haina mbadala.

Matotay alisema iwapo serikali itakuwa na utaratibu huo wa kutenga asilimia fulani mapato yote na kuwekwa kwenye mfuko huo itakuwa na uhakika wa fedha za kuhudumia Sekta ya Afya kwa kiwango kikubwa.

"Bado kuna changamoto kwenye upatikanaji wa huduma bora za afya na hiyo inatokana na ufinyu wa bajeti. Mfano Bajeti ya mwaka 2018/19 ya afya kiasi kilichotengwa hakikutolewa kama ilivyopitishwa, bali kilichotolewa ni asilimia 39 tu ya bajeti, sasa hatuwezi kufikia malengo kwa asilimia hiyo ya fedha," alisema.

Matotay alisema IRCPT katika mikutano yao mbalimbali nchini wamefanya utafiti na kuona upo umuhimu wa serikali kuangalia upya mfumo wa ukusanyaji mapato yake kwa kutenga asilimia kadhaa ya mapato yote ya taifa na kuwaweka katika mfuko maalum wa afya ili kuhakikisha sekta hiyo haikwami katika kutoka huduma bora za afya.

"Zipo nchi zinatumia mfumo huu wa kutenga asilimia kadhaa ya mapato yake na kuyaweka kwenye mfuko wa afya, wamefanya hivi kwa sababu afya haina mbadala," alisema.

Nizar Utanga, Ofisa Mawasiliano wa Norwegian Church Aid, alisema kuna haja jamii kushiriki kikamilifu katika kufuatilia matumizi ya fedha zinazotolewa kwa ajili ya huduma za afya.



Nipashe

MWANGA WA JAMII

# Kasi ya urasimishaji, upimaji ardhi iongezeke

**KASI** ya urasimishaji na upimaji wa ardhi bado siyo ya kuridhisha kwenye majiji, miji na vijijini, jambo linalotoa hofu kuwa ukuaji hauendani sawa na utendaji wa serikali.

Mathalani, Jiji la Dar es Salaam ambalo linakua kwa kasi, huku urasimishaji na kupima ardhi ukiwa na kasi ndogo, kuna uwezekano mkubwa kuwa na maeneo yasiyopangwa.

Tunatambua kazi kubwa inayofanywa ya kurasimisha makazi mengi ambayo hayakupimwa na kuwa na ujenzi holela, lakini bado changamoto ni kubwa.

Ukienda nje ya jiji hilo kuna ujenzi unaendelea, lakini haufuati taratibu na mbaya zaidi serikali za mitaa hazijafanya kazi yake ipasavyo, ikiwamo kuchukua rushwa kwa wananchi.

Aidha, kumekuwa na changamoto kwa maofisa ardhi kutoa vibali vya ujenzi kwa wakati, jambo linalosababisha watu kujenga bila kufuata utaratibu na kuondoa muonekano wa jiji, mji au vijiji.

Hakuna ubishi kuwa urasimishaji ardhi una faida za kiuchumi kwa kuwa mwananchi atatumia ardhi au kilichopo kwenye ardhi yake kupata fedha na kuendeleza maisha yake.

Ardhi ya namna hiyo inakuwa imeongezewa thamani itaisaidia jamii, na kubwa zaidi mji uliopangwa utakuwa na mwonekano mzuri na sahihi.

Jana Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, iliwasilisha Makadirio ya Mapato ya Matumizi kwa mwaka 2021/22, na moja ya mkakati mkuu ni urasimishaji makazi na kupima kila kipande cha ardhi.

Malengo ni kutambua, kupanga, kupima na kumilikisha vipande vya ardhi milioni 2.5 kwa mijini na kutoa hatimili za kimila milioni 2.6 kwa vijijini.

Tangu serikali ya awamu ya tatu kulikuwa na mpango wa kuhakikisha kila kipande cha ardhi kimepimwa, na kuwa na mpango bora wa matumizi ya ardhi ili kupunguza migogoro na kuongeza thamani ya ardhi, lakini mafanikio ni kidogo na sasa tunataka kuona kasi hiyo.

Kwa mfano, kuna migogoro kati ya wakulima na wafugaji, maeneo yaliyo hifadhiwa na wananchi waishio jirani, lakini hiyo ni kutokana na kukosekana kwa mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Kwamba ardhi ya kijiji au eneo ipangwe na kila kipande kiwe na matumizi yake kwa maaana ya eneo la malisho, eneo la hifadhi ya mazingira, huduma za jamii kama shule, zahanati, makaburi, makazi ya watu na maeneo ya kilimo.

Lakini kupanga miji kwamba kusiwe na ujenzi holela na utaratibu sasa wa ujenzi kuanzia aina ya nyumba na mapaa, ili kuondokana na kila mtu kujenga kwa kadiri ya misuli yake ya fedha.

Unapotembelea majiji mengi duniani tangu ukiwa angani, unaona jinsi ilivyopangwa kiasi cha kuongeza thamani na kupendezesha, lakini kwa Tanzania ni kawaida kukuta ghorofa refu, fupi, nyumba za kawaida katika eneo moja.

Kama huko nyuma yaishafanyika makosa, ni muhimu sasa yakarekebishwa kwa ujenzi unaoendelea ili kuwe na miji iliyopangwa vizuri.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:


**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Mitihani itungwe na wanaohusika, siyo kumsukumia kila aliye jirani



Na Yasmine Protace

**TUNAPOZUNGUMZIA** suala la mitihani, tunamaanisha watu wanafanya mitihani, ikiwa ni tathmini kwa ajili ya jambo fulani. masomoni, huwa kuna mitihani ya ama kutathmini daraja la kuvuka ngazi moja kwenda nyingine au kuhitimu.

Pia kuna mitihani ambayo mtu anafanya kwa ajili ya kuhamia shule nyingine, au kuhitimu ngazi fulani ya masomo. Kwa ujumla wake, kuna mengi.

Kwa ujumla, takriban mitihani yote inayofanyika inatungwa na walimu wa masomo husika, kupitia usimamizi wa mamlaka stahiki.

Cha kushangaza ni ushuhuda wa tukio, baadhi ya walimu wanaingiwa na uvivu wa kushindwa kutunga mitihani, badala yake wanakaimu jukumu kuwataka wengine nje ya stadi watungie. Ni kosa kila mwalimu anapotunga mitihani kutokana na maudhui anayowafundisha wanafunzi.

Hivi karibuni serikali ilipiga marufuku kwa asiye na sifa za ualimu, kuwatungia wanafunzi mitihani ya majaribio au ya kupanda madarasa mapya.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abdully Maulid, alikuwa mgeni rasmi, alitamka hayo katika Mahafali ya 13 ya Ualimu katika Chuo cha Ebonite, Kimara, jijini Dar es Salaam.

Maulid anasema kuna baadhi ya walimu wanaoshindwa kuwatungia mitihani wanafunzi wao na kuwaachia wasio na sifa za kuitunga mitihani hiyo.

"Haya mambo ya watu wasio na sifa za ualimu kutunga mitihani naona yameanza miaka ya siku hizi. Zamani hayakuwapo, sasa mwalimu akitungiwa mitihani na mtu baki ajue atachukuliwa hatua za kisheria," anaonya.

Anasema mitihani inatungwa na walimu

kutokana na ufundishaji wao. Pia Baraza la Mitihani la Taifa (NEC), nalo ni chombo rasmi cha kutunga mitihani.

Pia anawataka wahitimu wote wa mafunzo ya ualimu, wasikae mitaani, badala yake waombe kazi katika shule zilizo jirani nao, mwenyewe ambaye ni mwanataaluma hiyo, anawaasa:

"Hapa wanaohitimu wote wa Ebonite mmeshinda mitihani yenu. Sasa mnatakiwa kuomba kujitolea kufundisha katika shule mlizo nazo karibu, ili kuondokana na usumbufu wa nauli."

Anawageukia waajiri kwa kuwataka wakuchukue walimu wenye sifa stahiki na huku 'kuwapigia debe' waajiriwe waliomaliza katika chuo cha Ebonite, anayoipongeza kwa ufanisi wake. Pamoja na kuibuka kwa maradhi ya Covid - 19 mwaka jana, anaisifu shule hiyo kuweza kuwajali walimu wake, kwa kuendelea kuwalipa mishahara yao.

Anasema zipo taasisi ambazo baada ya kuwapo janga la corona, zilishindwa kuwalipa mishahara wafanyakazi waona na hata baadhi ya mitaala kubadilika, bado hakuna kasoro kwa wanafunzi.

Anaongeza kuwa kila mwalimu anatakiwa kuwafundisha wanafunzi somo analolielewa yeye, katika mitihani wa mwaka huu wa darasa la saba utakaofanywa kwa mtindo mpya.

Maulid anasema, msimamizi atasoma notisi, akimaliza atamwambia mtoto ajaze yale akiyoyaelewa kupitia notisi alizosoma, akifafanua kuwa serikali inawajali walimu na ndio maana imenunua magari 184, ili yawasaidie.

Makamu Mkuu wa chuo hicho, Lusajo Mwaigosya, anasema chuo kilianzishwa mwaka 2007 kwa kutoa huduma za ualimu kwa ngazi mbalimbali na mwaka 2015 walipewa cheti cha ubora, kutokana na kutoa elimu bora.

Anasema mipango ya chuo kwa sasa, ni kuanzisha elimu maalumu, ikiwamo kuanzisha kituo cha ufundishaji lugha za Kichina na Kifaransa, mpango ulioko katika hatua mbalimbali. Mwaigosya anaoinba serikali kusikia, anaongeza kwamba hivi sasa wanaiomba serikali udahili katika vyuo binafsi, uwe kuanzia pointi 26.

Anaongeza kuwa serikali itazame pia suala la kodi, kwa kuwapunguzia mzigo wawekezaji hali hiyo inachangia watu wanashindwa kuviendeleza vyuo hivyo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Ebonite, Thadeus Njuu, anasema kuwa katika mahafali hayo, wahitimu zaidi ya 100 wamehitimu mafunzo mbalimbali ya ualimu.

Anasema kuwa, wahitimu wanapoenda kufundisha huko wawe mabalozi wazuri katika utoaji elimu na walimu wanaoanza kazi wawe makini na masomo wanayofundisha na kuongeza juhudi katika ufundishaji.

Anaasa walimu wawapende watoto wanapowafundisha, ili nao wamudu kumwelewa mwalimu, hata wakafanya vyema.

Anasema watoto wasichapwe ovyo, bali kuna taratibu zake.

# NIT yazindua kituo cha mafunzo ya anga

**Na Maulid Mmbaga**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), kimezindua rasmi kituo cha umahiri cha mafunzo ya taaluma za usafiri wa anga na operesheni za usafirishaji sambamba na kamati ya ushauri ya wadau wa kisekta watakaoshirikiana katika kuboresha ufanisi wa kituo hicho.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa chuo hicho, Prof. Zacharia Mganilwa, wakati wa uzinduzi huo uliofanyika jana katika chuo hicho Mabibo mkoani Dar es Salaam, ambapo alieleza kuwa kituo hicho ni cha kihistoria, kwani ni muhimu katika sekta ya usafirishaji na kilianzishwa na mradi wa (EASTRIP) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Alisema ili kuimarisha uhusiano wa vyuo na wadau wa sekta na kuhakikisha kuwa mafunzo yatakayotolewa yanakidhi mahitaji ya soko, Benki ya Dunia ilielekeza vituo vyote vya umahiri kuwa na kamati ya ushauri wa wadau wa kisekta waliobobea katika kufundisha njia zote za usafirishaji.

"Asilimia 50 ya wajumbe wa kamati hiyo wametoka sekta binafsi na majukumu yao ni kutoa mapendekezo na ushauri utakaosaidia kituo kukidhi mahitaji ya elimu bora ya ufundi ndani na nje ya nchi," alisema.

Aliongeza kuwa kupitia EASTRIP, chuo kitapata zaidi ya Sh. 49,053,500,000 kwa ajili ya kuanzisha kituo hicho, na kitasaidia kupunguza uhaba wa wataalamu katika sekta ya usafiri wa anga.

Alisema kupitia fedha hizo, chuo kitatoa udhamini (scholarships) kwa wanafunzi wasichana kuwawezesha kusoma na kubobea katika taaluma za anga na logistiki, kuboresha na kutengeneza mitaala inayokidhi mahitaji ya soko la ndani na nje.

Alibainisha kuwa kituo kitaweza kutoa wahitimu wa mafunzo ya taaluma za anga na operesheni za usafirishaji zaidi ya 4000 katika kipindi cha miaka mitano ya mradi pamoja na kuongeza uwezo wa waalimu kupitia mafunzo ya shahada za uzamili, mafunzo ya muda mfupi na mafunzo ya vitendo.

"Katika mradi huu tutaweza kuboresha miundombinu kwa kujenga majengo tisa ikiwamo jengo la kituo cha umahiri Mabibo, mock up, la mafunzo ya ufundi, hosteli mbili zenye kubeba wanafunzi 2,100, anga ya ndege Dar es Salaam, anga ya ndege Kilimanjaro, makazi ya wafanyakazi Kilimanjaro na makazi ya wanafunzi Kilimanjaro," alisema.



Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Emmanuel Tutuba (kulia) na Nnenna Nwabufo, Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, Kanda ya Afrika Mashariki, wakibadilishana baada ya kitia saini mikataba miwili ya mkopo yenye thamani ya dola za Marekani milioni 140 (takriban shilingi bilioni 323.4) kwa ajili ya kufadhili Mradi wa kufua Umeme wa Mto Malagarasi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: WFM**

# ADB yaikopesha Tanzania bil. 323/-

**Na Enock Charles**

SERIKALI imetia saini mkataba wa mkopo wa Dola za Marekani milioni 140 (sawa na Sh. bilioni 323), kwa ajili ya kufadhili mradi wa kufua umeme wa Mto Malagarasi kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) ili kutekeleza sera ya taifa ya nishati ya mwaka 2015.

Akizungumza katika hafla ya utiaji saini jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, alisema mradi huo utahusisha ujenzi wa kituo kipya cha uzalishaji wa umeme wa gridi ya 495 MW chenye uwezo wa kuzalisha Gwh 181 za umeme kwa mwaka.

"Utekelezaji wa mradi unalenga kuboresha usambazaji wa umeme katika mikoa ya magharibi mwa Tanzania ili kuchangia mabadiliko ya kijamii na kiuchumi nchini na kusaidia katika jitihada za kupunguza umaskini," alisema Tutuba.

Mradi huo unaotarajiwa kuchukua miaka mitano, utajumuisha ujenzi wa kituo cha umeme wa maji kupitia ujenzi wa bwawa, ujenzi wa barabara za kuingia eneo la mradi, madaraja na kambi za kudumu pamoja na ofisi na nyumba za wafanyakazi, zahanati, shule za msingi, kazi za mitambo ya elektroniki inayohusika na uzalishaji na usambazaji umeme na upandaji miti.

Pia alisema pamoja na ujenzi wa kituo cha uzalishaji umeme, mradi huo utajumuisha ujenzi wa njia ya usafirishaji umeme, upanuzi wa mtandao wa usambazaji wa umeme vijijini ili kuongeza uwezo wa kusambaza umeme kwa wananchi, ununuzi wa transfoma mpya 15 na kuijengea TANESCO uwezo wa kitaasisi.

Mkurugenzi wa benki hiyo Afrika Mashariki, Nnenna Nwabufo, alisema imekuwa ikifadhili miradi mbalimbali nchini na miaka mitatu tu iliyopita ilipitisha ufadhili wa miradi iliyogharimu jumla ya Dola bilioni 1.12 ikiwamo ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Msalato jijini Dodoma na barabara katika jiji hilo.

Alisema jumla ya miradi inayoendelea waliofadhiliwa Tanzania ina thamani ya Dola bilioni 2.33, ikiwa inalenga sekta muhimu kama usafirishaji, umeme, maji na kilimo.

# Mashine iliyozama bandarini yaopolewa

**Na Christina Mwakangale**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari (TPA) imefanikiwa kuiopoa mashine ya kunyanyua vitu vizito (crane) iliyozama Mei 23, mwaka huu, kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Elihuruma Lema, alisema jana kuwa mashine hiyo yenye uzito wa takribani tani 70, iliopolewa juzi jioni.

"Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania inaujulisha umma kuwa Jumatatu Mei 24, mwaka huu, majira ya saa 12:20 jioni, zoezi la kuopoa mashine ya kunyanyua vitu vizito 'crane' iliyotumbukia baharini limekamilika," alisema Lema katika taarifa yake hiyo ya jana.

Alisema mashine hiyo ilipata ajali ya kutumbukia majini katika eneo la Gati ya Malindi, ilipokuwa inashushwa kutoka kwenye Meli ya LCT AJE 1 baada ya kuwasili Bandari ya Dar es Salaam ikitokea visiwa vya Songosongo.

"Mamlaka inawashukuru wataalamu wake wazalendo waliofanikisha kutokana na weledi wao wa hali ya juu pamoja na wadau wote kwa utulivu wao wakati wote wa kukabiliana na tukio hili," alisema.

Juzi, Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa TPA, Nicodemus Mushi, alisema uopoaji wa mashine hiyo ulianza kwa kutumia vifaa maalum na wazamiaji.

"Tuna uwezo wa kuiopoa crane hii yenye uzito wa tani 70, vifaa vyetu vina uwezo wa kuopoa hata mzigo wa tani 100, tunazo mashine za kubeba vitu vizito 'gottwald cranes', iwapo kitu kizito kikizama baharini.

"Crane ilizama wakati ikishushwa na kutumbukia baharini, mashine hiyo ni mzigo wa mteja na meli pia si ya kwetu," alisema Mushi.

Katika taarifa yake ya jana, TPA ilisema ajali hiyo haikusababisha madhara yoyote kwa watu huku ikiwaondoa hofu wateja wake.

**HABARI KITAIFA**

## Kituo chenye mahakama 4 kujengwa kwa bil. 8.5/-

**Na Richard Makore,** MWANZA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 8.5 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki (IJC) ambacho kitakuwa na mahakama nne jijini Mwanza.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Mwanza jana, Mhandisi wa Mahakama ya Tanzania, Fabian Kwegirwa, alisema ujenzi huo ulianza mwaka jana na unatarajia kukamilika Desemba mwaka huu.

Alisema jengo litakuwa na mahakama ya mwanzo, wilaya, hakimu mkazi na mahakama kuu na ujenzi wake umefikia asilimia 58.

Aidha, alisema katika jengo hilo kutakuwa na kumbi mbalimbali kwa ajili ya kusikiliza kesi, sehemu ya mahabusu, eneo la kusikiliza kesi za watoto pamoja na ofisi za majaji na mahakimu.

Kwegirwa alisema jengo hilo la kisasa limezingatia vigezo vyote vya kiusalama pamoja na ubora na kwamba Sh. bilioni 8.5 zitatumika hadi kukamilika kwake.

Aliongeza kuwa mambo yaliyozingatiwa katika ujenzi huo ni pamoja na mifumo mbalimbali inayotumia teknolojia ya kisasa, usalama kwa watumiaji wa mahakama na urahisi wa wananchi kufika katika jengo na kupata huduma.

Kituo hicho kilichojengwa eneo la Buswelo jijini Mwanza ni miongoni mwa vituo vitano kama hivyo vinavyoendelea kujengwa hapa nchini.

Mkandarasi anayejenga jengo hilo, Chacha Fednand, alishukuru serikali kwa kuiamini kampuni ya kitanzania na kuipa kazi hiyo.




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, akikabidhi tuzo ya udhamini kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Tigo, Simon Karikari, wakati wa hitimisho la kongamano la Wiki ya Ubunifu Tanzania 2021, jijini Dar es Salaam, lililokuwa na kauli mbiu ya "Ubunifu kwa Uchumi wa Kidijitali Stahimilivu na Shirikishi". **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## NHC kuwakabidhi watumishi nyumba 300

**Na Christina Mwakangale**

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC), linatarajia kukabidhi mradi wa nyumba 300 zenye thamani ya shilingi bilioni 14.4 kwa watumishi wa umma, zinazojengwa eneo la Iyumbu, Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma, ifikapo Juni mwaka huu.

Mradi huo wa ujenzi unatekelezwa kwa awamu tatu, utajenga nyumba 1,000 katika makao makuu ya nchi.

Mkurugenzi wa Uhandisi na Ujenzi wa NHC, Haikameni Mlekio, alisema watu wanaweza kuomba mikopo kupitia Benki ya Azania nyumba hizo 300 kwa ajili ya makazi na kupangisha.

Alisema awamu ya pili ya mradi huo, utahusisha ujenzi wa nyumba 325 pamoja na majengo sita ya huduma, na kwamba nyumba 275 zitajengwa katika awamu ya mwisho.

NHC inamiliki leseni ya daraja la kwanza la ukandarasi kwa ajili ya ujenzi wa miradi mikubwa ya shirika na hupokea pia kandarasi za nje.

Meneja Habari na Uhusiano wa NHC, Muungano Saguya, alisema, shirika hilo limefanikisha ujenzi wa majengo manne ya wizara nne katika eneo la mji wa serikali la Mtumba, uliogharimu shilingi bilioni 3.99.

Alisema gharama za ujenzi wa majengo hayo ni pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Fedha na Mipango; Viwanda na Biashara na Wizara ya Nishati.

Saguya alisema NHC pia ilimilikisha makao makuu ya EWURA jijini Dodoma kwa gharama ya shilingi bilioni 7.7.

"Ujenzi mwingine uliofanywa na NHC kama mkandarasi, ni jengo la halmashauri ya wilaya ya Malinyi kwa Sh. Bil. 2.74 na makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe Sh. Bil. 2.74 na machinjio ya kisasa ya Vingunguti jijini Dar es Salaam kwa shilingi bilioni 12.49," alisema Saguya.

Alibainisha kwa sasa, NHC inaendelea na ujenzi wa ofisi ya Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TDMA), Kanda ya Kati unaotarajiwa kukamilika, Juni mwaka huu.

## Ulega autaka ushirika matumizi vyema boti za mikopo ya TADB

**Na Mwandishi Wetu, S**ENGEREMA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi Abdallah Ulega, amekitaka Chama cha Ushirika cha Zilagula wilayani hapa kutumia vyema mkopo uliotolewa na

Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) kujenga boti za kisasa, ili zisaidie viwanda vya samaki jijini Mwanza kupata malighafi kwa wakati na kwa uhakika.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, baada ya

kuridhishwa na ujenzi wa boti tatu za kisasa za uvuvi, kati ya boti

tano ambazo zinajengwa kwa mkopo wa Sh. milioni 100.7 ambao umetolewa

TADB kwa chama hicho, Ulega alisema fedha hiyo ni mkakati wa serikali wa kuwapatia wavuvi vyombo vya kisasa na kwamba matumizi mazuri ya boti hizo utavifanya viwanda kupata malighafi kwa uhakika na

pia kuifanya sekta ya uvuvi kutoa mchango mkubwa zaidi kwenye pato la taifa.

"Mpango wa serikali ni kuona sekta ya uvuvi inatoa mchango zaidi katika ukuaji wa pato la taifa na ndiyo ili muweze kupata boti za kisasa zitakazowasaidia kufanya vyema shughuli zenu," aliwaeleza wanaushirika hao na kuongeza ni vyema mkopo huo ukatumika vizuri na marejesho yake yafanyike kwa

wakati.

"Kilio cha wavuvi wengi ni walanguzi wanaowanyonya. Walanguzi wamekuwa wanufaikaji wakubwa wa nguvu ya mvuvi. Uwapo wa boti hizi utawezesha kupata samaki wengi zaidi ambao watauzwa kwa bei nzuri kwa sababu samaki wanahitajika katika soko la ndani na nje ya nchi," alieleza.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alisema benki yao itaendelea kufanyia kazi changamoto zote zinazojitokeza ikiwamo kukosekana kwa mikopo kwa baadhi ya vyama vya ushirika licha ya kufuata taratibu zinazotakiwa.

"Mwanzoni tuliwaomba wavuvi waunde vyama vya ushirika ili tuweze

kuwapa mikopo. Tunashukuru kwa sababu mwitikio umekuwa mkubwa na hivyo kurahisisha kazi ya kuratibu mikopo inayotolewa na benki," alisema.

HABARI KITAIFA

# Jenerali Mbuge ataka ushirikiano wa taasisi

**Na Restuta Damian,** BUKOBA.

MKUU wa Mkoa Kagera, Meja Jenerali Charles Mbuge, amezitaka idara na taasisi mkoani humo kuacha ubinafsi na kuungana kutatua matatizo ya wananchi.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akikabidhiwa ofisi na aliyekuwa Mkuu wa mkoa huo kabla ya kuteuliwa kuwa Mkuu wa mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti.

Meja Jenerali Mbuge alisema uwazi na usimamizi wa haki katika shughuli pamoja na umoja kutasaidia kuleta maendeleo ya wananchi.

''Muungano huo huleta maendeleo kwa wananchi na kufanikisha kufikia lengo la kuwa na uchumi wa kati na kuzitambua fursa kwenye maeneo mbalimbali,'' alisema.

Alisema uchumi wa mkoa unategemea usalama kwa wananchi kutoruhusu kuingiza mtu nchini bila kufuata utaratibu wa kusheria.

Awali akizungumza baada ya makabidhiano, Brigedia Jenerali Gaguti, alisema viongozi wa dini wana nafasi kubwa katika kulinda amani kwa kushirikiana na kamati ya usalama na wananchi.

# Nachingwea yajikomboa kwa madarasa sekondari

**Na Sabato Kasika,** NACHINGWEA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, imesema wanafunzi wote watakaochaguliwa kidato cha kwanza mwaka ujao, wataanza masomo kwa pamoja, kwa kuwa hakutakuwa na uhaba wa madarasa.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Hassan Rugwa, katika hafla ya kupokea mifuko 1,800 ya saruji iliyotolewa na Mbunge wa Nachingwea, Dk. Amandus Chinguile, kwa ajili ya sekondari 16 za kata.

"Tuna uhaba wa madarasa 22 katika shule 16, lakini ninaamini wanafunzi wote watakaochaguliwa kuingia kidato cha kwanza, wataanza masomo pamoja, kwani tatizo la uhaba wa madarasa litakuwa limeisha," alisema Rugwa.

Alisema, mahitaji yao ni mfuko 1,320 ya saruji kwa ajili ya idadi hiyo ya madarasa, lakini wamepokea 1,800 ya mbunge, na kwamba huo ni mwanzo mzuri unaoonyesha kuwa lengo la kumaliza tatizo hilo litatimia.

Alifafanua kuwa, mbali na mifuko hiyo ya saruji waliopata, wapo wadau wengine walioahidi kusaidia ujenzi wa madarasa, hali inayompa matumaini kuwa hakuna wanafunzi watakaokosa madarasa.

# Walimu wapewa somo la uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WALIMU wametakiwa kuwekeza na kujiendeleza katika kukopa mikopo nafuu yenye tija ya kutatua changamoto zinazowakabili ili kunufaika na kufurahia kazi wanayoifanya.

Hayo yalisemwa na Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, katika mafunzo ya walimu wa mkoani hapo yaliyoandaliwa na Benki ya NMB ambaye ni Ofisa Elimu (Sekondari), ,Khalifani Omary, na kwamba mafunzo hayo yatawajenga walimu katika kujiwekea kipato ili kujiendeleza kimaisha.

"Mafunzo haya yatawasaidia katika kuwaongezea elimu na kutoa fursa ya maoni namna wanavyoweza kunufaika na benki ya NMB ikiwa jitihada hizi zitaleta matokeo chanya na kuleta faraja kwa jamii," alisema Omary.

Alisema jitihada hizo ni nzuri na zinaunga mkono juhudi za serikali katika kuhakikisha Watanzania walio wengi wanajumuhishwa katika mfumo rasmi wa kifedha ili kuinua vipato vyao na kiuchumi kwa ujumla, hivyo alitoa rai kwa taasisi nyingine za kifedha nchini kufanya jitihada hizo kama NMB.

Alishukuru benki hiyo kwa kuboreshwa huduma za kibenki na kusogezwa karibu na wateja wake, kwani awali walimu walipata taabu kutembea umbali mrefu, hivyo benki ya NMB imekuwa chachu ya maendeleo katika jamii kwa kuwanufaika wateja wake. Mkuu wa biashara za kadi wa benki ya NMB, Philbert Casmir, alisema wameandaa mafunzo yanayoitwa siku ya walimu ambapo wameanza mkoani Arusha kwa kutambua mchango wa mwalimu katika jamii na kutoa suluhisho la changamoto zao katika kujikwamua kimaisha ikiwamo mikopo nafuu na bima mbalimbali.

"Tunatambua mwalimu ni mwezeshaji katika jamii, hivyo NMB tumekuja na muundo wa kutokutoa bidhaa au suluhisho ya maisha ya walimu, kwani tunatambua kunachangamoto za ujenzi na kupitia mafunzo haya wataelimishwa na kutumia mikopo nafuu ya NMB kujiendeleza katika suala la ujenzi wa nyumba," alisema.

Casmir alisema pia kuna bima za walimu na Watanzania kwa ujumla zinazoweza kuwasaidia kupata fedha pamoja na hilo pia kunachangamoto ya elimu ya fedha watu kutoweka fedha katika taasisi za kibenki na kutunza majumbani, hivyo elimu hiyo itawasaidia kufikisha ujumbe na faida za kuweka fedha benki.

Baadhi ya walimu hao waliishukuru benki hiyo kwa kuwapa mafunzo ambayo yatawasaidia katika kuweka fedha na kutumia katika matumizi sahihi ya kujiendeleza kiuchumi.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Daraja mbili, Zukra Kalunde, alisema mafunzo hayo yatawasaidia katika kufahamu umuhimu wa kadi pamoja na kujifunza namna ya kupata mikopo nafuu ya benki hiyo itakayowasadia kujiendeleza kiuchumi kama ujenzi wa nyumba zao za kuishi na biashara.



Walimu wakuu wa shule za msingi na sekondari mkoani Arusha, wakifuatilia uzinduzi wa semina ya mafunzo ya bidhaa za Benki ya NMB, wakati wa hotuba ya mgeni rasimi, kwenye uzinduzi wa semina ya mafunzo ya elimu ya fedha na bidhaa za NMB, jijini Arusha jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wenye ulemavu waitwa mikopo ya halmashauri

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, Anderson Msumba, amewataka watu wenye ulemavu, kuchangamkia fedha za mikopo asilimia mbili, ambazo hutolewa kwa ajili ya kuwakwamua kiuchumi.

Alisema katika mwaka wa fedha 2020/2021, halmashauri hiyo ilishatenga kiasi cha fedha Sh. bilioni 1.4 kwa ajili ya utoaji fedha za mikopo asilimia 10, ambapo nne kwa vijana, nne wanawake na mbili kwa watu wenye ulemavu.

Msumba alibainisha hayo juzi, akisema wameshapokea maelekezo kutoka wizarani kutoa fedha za mikopo kwa watu wenye ulemavu kuanzia mtu moja, na siyo lazima kuwa kwenye kikundi kama zamani na kuwataka watu hao wajitokeze kwa wingi kupata mikopo hiyo ili wajikwamue kiuchumi. "Mwitikio wa watu wenye ulemavu kuja kuomba fedha za mikopo kwenye manispaa yetu ni mdogo sana ukilinganisha na kundi la wanawake na vijana, hivyo nawaomba wajitokeze kwa wingi kuja kupata fedha hizi na kujikwamua kiuchumi," alisema Msumba.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii Manispaa hiyo, Robert Kwela, alisema wameshaandaa utaratibu wa kutoa elimu ya ujasiriamali kwa kundi hilo la watu wenye ulemavu, ili wapate mbinu za kufanya biashara na kuacha kuwategemezi na kuomba misaada. Mwenyekiti wa Shirikisho la Chama cha Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) wilayani Kahama, Michael Makanjiwa, alisema wanasuasua kuomba mikopo kwa sababu hawana elimu ya ujasiriamali na kuipongeza serikali kutaka kuwapatia elimu hiyo, ambayo itakuwa mkombozi kwao.

# Serikali yafunguka uhaba mafuta ya kula

BUNGE limeelezwa kuwa Tanzania inakabiliwa na upungufu wa mafuta ya kula metric tani 400,000, na kwamba serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwamo kukaa na sekta binafsi na Wakala wa Mbegu za Kilimo( ASA) ili kuzalisha mbegu za kutosha.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Stella Fiyao.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali imejipangaje kuleta mbegu bora ya alizeti kwa bei ya chini ili kila mtu aweze kumudu na kusaidia kuondokana na upungufu wa mafuta ya kula.

Akijibu, Bashe alisema mahitaji ya mbegu ni kati ya metric tani 5000-6000 na zitazalishwa kwenye eneo lenye hekari milioni 1.3 na kwamba hatua hiyo itawezesha uzalishaji wa tani zaidi ya milioni 1.2 ya mbegu zitakazokwenda viwandani.

"Hatua tunazochukua uzalishaji wa ndani tutazalisha tani 2,000, tunakaa na ASA na waagizaji wa nje, tutaagiza upungufu wa mbegu mwaka huu na tutapeleka kwa wakulima na bei itashuka kutoka Sh.30,000 ili ifike Sh.7000 kwa kilo moja, Wizara itasimamia suala hilo ili mbegu zipatikane kwa bei nafuu," alisema.

Katika swali lake la msingi, Mbunge huyo alihoji ni lini serikali italeta pembejeo za kilimo kwa bei nafuu ambayo wakulima wengi wataweza kuimudu.

Bashe akijibu, alisema serikali inalo jukumu la kuratibu mahitaji ya pembejeo kutoka kila Mkoa na kuweka mazingira wezeshi kwa kampuni kupeleka na kuuza kwa wakulima pembejeo zenye ubora, kwa wakati na kwa bei nafuu kwa kutumia mifumo mbalimbali ikiwamo Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja ambao huratibiwa kwa kudhibiti bei ili mkulima apate pembejeo hiyo kwa bei nafuu.

Hata hivyo, alisema katika kipindi cha miaka minne tangu kuanzishwa kwa mfumo huo bei za ununuzi kwenye chanzo zimepungua kwa asilimia 6 hadi 17 kutegemeana na aina ya mbolea na gharama za kuisafirisha baharini.

Alisema zimepungua kutoka Sh. 23,000 kabla ya FBPS hadi Sh. 2,800 kwa zabuni iliyofanyika tarehe 25 Juni, 2020.

"Aidha, bei za mbolea ya DAP na UREA katika soko la ndani zimepungua kwa asilimia 11 hadi 40 kutegemea jiografia ya eneo husika,"alisema.

Aidha, alisema serikali inaendelea kutekeleza mikakati ya kuongeza upatikanaji wa pembejeo kwa kuvutia wawekezaji wa kampuni binafsi za mbegu kuingia mikataba maalum na ASA kuzalisha mbegu bora kwa kutumia baadhi ya mashamba ya Serikali yanayomilikiwa na wakala ili kurahisisha upatikanaji wake.

"Kuboresha miundombinu ya barabara na reli ili kurahisisha usafirishaji wa pembejeo kutoka eneo moja kwenda jingine. Kwa kutumia njia ya reli, gharama ya usafirishaji hupungua kwa asilimia 60 na kusafirisha mbolea nyingi kwa muda mfupi ikilinganishwa na njia ya barabara," alisema.

Alitaja mikakati mingine ni kuwahamasisha wakulima kupitia Vyama vya Ushirika kutumia letter of credit kwa gharama isiyozidi asilimia 2 badala ya kutoa dhamana asilimia 20 ya mikopo wanayochukua kwa ajili ya kununua pembejeo na kupunguza na au kufuta baadhi ya tozo na ada kwenye pembejeo ambapo kati ya mwaka 2015 na 2020.

Alisema serikali imepitia na kufuta tozo na ada 12 katika mbegu na tozo nne za mbolea ili kupunguza bei na gharama za pembejeo hizo.



Mbunge wa Viti Maalumu (CHADEMA), Halima Mdee, akichangia hotuba ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2021/2022 ilipowasilishwa Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## TARURA kutathmini barabara zake zote

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema katika mwaka wa fedha 2021/22, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijin i(TARURA) umepanga kufanya tathmini ya miundombinu ya barabara zake zote, ikiwamo za Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ili kuandaa mpango wa namna bora ya kutoa vipaumbele vya ujenzi na matengenezo ya barabara na madaraja.

Pia, kwa mwaka wa fedha 2020/21, TARURA Chemba imetenga Sh. milioni 84.04 kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Kwamtoro – Sanzawa – Mpendo yenye urefu wa kilomita 23.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, David Silinde, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Chemba (CCM), Mohamed Monni.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji ni lini Barabara ya Kwamtoro – Sanzawa – Mpendo yenye kilomita 58.2 itajengwa kwa kiwango cha kupitika msimu mzima kwani kwa sasa imekatika kwa sababu ya mvua kubwa na kutojengwa kwa muda mrefu.

Akijibu, Naibu Waziri Silinde alisema ujenzi wa barabara hii unaendelea ambapo matengenezo ya barabara yenye urefu wa kilomita 10, makalvati 2 na drift moja umekamilika.

Alieleza katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya Sh. milioni 42 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara yenye urefu wa kilomita 10 na ujenzi wa makalavati 3.

Aidha, alisema serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya barabara ikiwemo ya barabara ya Kwamtoro – Sanzawa – Mpendo kadri ya upatikanaji wa fedha ili kuimarisha usafiri na usafirishaji.

# 'Zege teknolojia mbadala ujenzi mashimo ya migodi'

SERIKALI imesema teknolojia mbadala ya ujenzi wa mashimo ya migodi kwa kutumia zege na nondo ni salama na haina athari kubwa za kimazingira ukilinganisha na matumizi ya magogo.

Naibu Waziri wa Madini, Prof. Shukrani Manya, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Ghati Chomete.

Katika swali lake, Mbunge huyo alitaka kujua serikali ina teknolojia gani mbadala ambayo itaepusha kutumia magogo kama matimba kwenye mashimo ya migodi hasa maeneo ya Nyamongo, Tarime,Buhemba na Butiama.

Akijibu swali hilo, Prof. Manya alikiri wachimbaji wengi wadogo katika maeneo mbalimbali yenye shughuli za uchimbaji wa dhahabu yakiwemo maeneo ya Nyamongo, Tarime, Buhemba na Butiama wamekuwa wakitumia magogo (matimba) kama njia ya mihimili ulalo na wima kwenye mashimo ya migodi.

Alisema pamoja na teknolojia hiyo kuonekana kuwa ya gharama nafuu, imekuwa ikisababisha uharibifu mkubwa wa mazingira licha ya kuwa si salama na si ya kudumu.

Alibainisha teknolojia mbadala inayotumika kwa sasa ni ujenzi wa mashimo ya migodi kwa kutumia zege na nondo na haina athari kubwa kimazingira ikilinganishwa na matumizi ya magogo.

Alifafanua miongoni mwa sababu zinazopelekea wachimbaji wadogo kutotumia teknolojia hii ni ufinyu wa mitaji, kutokuwa na maeneo ya kudumu ya uchimbaji na baadhi yao kutokuwa na leseni za uchimbaji.

Alisema Serikali inaendelea kuwarasimisha wachimbaji wadogo kwa kuwapatia leseni za madini ili kutambulika kisheria na kuwawezesha kuaminika katika taasisi mbalimbali za fedha.

" Serikali kupitia STAMICO inaendelea kutoa elimu kwao kuhusu uchimbaji wa kitaalam na wenye tija unaozingatia masuala ya afya, usalama na utunzaji mazingira," alisema.




**Habari zote na Augusta Njoji, DODOMA**

Ukurasa 12

## MABADILIKO SEKTA YA MAJI: NYASA WAJIBIWA

Na Mwandishi wetu

Maji ni huduma muhimu katika maisha ya kila siku, hivyo maji ni uhai. Maendeleo yoyote yanahitaji huduma ya maji. Serikali kupitia Wizara ya Maji imeweka kipaumbele katika kuhakikisha huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza inamfikia mwananchi, maeneo ya mijini na vijijini. Wananchi ndio wadau wakuu wa serikali na wizara haitakuwa kikwazo katika kufanikisha huduma ya maji kwa wananchi.

Hatua hizo zinazochukuliwa na serikali zinalenga kuleta maendeleo kwa wananchi na kuwawezesha kutekeleza shughuli za kimaendeleo katika sekta nyingine na kujiongezea kipato.

Sasa wananchi wa vijiji vya Lundo, Lipingo na Ngindo wilayani Nyasa Mkoani Ruvuma wana kila sababu ya mapinduzi makubwa na kuondosha magonjwa ya mlipuko ambayo yanapotokea huwafanya wananchi kukosa utulivu katika utekelezaji wa shughuli za kiuchumi, na kazi nyingine za kuwaletea maendeleo.


"Naishukuru sana serikali na Wizara ya Maji kwa mradi huu ambao upo katika hatua za mwisho za utekelezaji, ni hakika serikali imewajibu wananchi kuhusu huduma ya maji na sasa tutapata utulivu kabisa tofauti na awali ambapo wananchi walihangaika", Mkuu wa Wilaya Nyasa Isabela Chillumba amesema.

Naye Maiko Gidion mnufaika wa mradi huo anasema ukosefu wa maji ulikuwa ni kilio kwa wananchi.

"Tunaishukuru serikali kwa kutupatia mradi huu na kufanikisha ujenzi wa vituo ishirini vya kuchotea maji wananchi katika kijiji chetu cha Lundo", Maiko Gidion anasema na



*Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) akijumuika na wataalam wa ufundi katika kuchanganganya udongo wa ujenzi (Zege) katika moja ya mradi wa maji hivi karibuni.*




# Lilivyokuwa baa la volkano, wenyeji kutawanyika mbio DRC hadi Rwanda

**Goma, DRC**

MAMA Ernestine Kabuo (68), alirudi nyumbani baada ya kukimbia mtiririko wa udongo wa volkano, maarufu lava huko Goma Mashariki, nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na kugundua mumewe alishafariki dunia.

Mama huyo alishindwa kumbeba mumewe mgonjwa kutoka nyumbani kwao na aliporudi alimkuta ameungua hadi kufa.

Huo ni mfano kwa takriban vifo 15 vilivyothibitishwa hadi juzi asubuhi, kutokana mlipuko wa volkano Jumamosi katika Mlima Nyiragongo.

Ni tukio la marudio, kwamba mwaka 2002, alishuhudia uharibifu mkubwa wilayani Buhene, ambako nyumba ya bibi huyo imo katika orodha.

Mama huyo anaendeleza simulizi ya alivyokabili mlipuko wa volkano katika kauli ya huzuni kwamba: "Nilijiambia, siwezi kwenda peke yangu, tumeoana kwa nyakati za furaha na huzuni.

"Nilirudi angalau kujaribu kumtoa lakini sikuweza. Nilikimbia na akaungua ndani. Sijui cha kufanya. Ninailaani siku hii."

Wakazi wengine wa Goma, mji wenye wakazi 670,000 kwa mujibu wa makadirio ay Umoja wa Mataifa wanaendelea kutafuta wapendwa wao waliopotea na eneo hilo linaendelea kushuhudia matetemeko ardhini.



Hali halisi ya athari za Volkano kutoka Mlima Nyarigongo, DRC wikiendi iliyopita. **PICHA: MTANDAO.**

Shirika la Umoja wa Mataifa la Watoto (UNICEF), linasema zaidi ya watoto 170 wanahofiwa kutoweka na wengine 150 wametengwa na familia. Sasa linasema jumla ya vituo vitaanzishwa kusaidia watoto walioachwa na wazazi wao.

Watu tisa kati ya watu 15 waliouawa, ni waliofariki katika ajali za barabarani walipokuwa wakimbia kunusuru maisha yao, kauli ambayo Jumapili iliyopita ilithibitishwa na Msemaji wa Serikali, Patrick Muyaya.

Tope hilo la Volkano lilirushwa mbali, hata hivyo nje kidogo ya jiji Goma, kufika mamia ya nyumba na majengo makubwa.

"Nyumba zote katika mtaa wa Buhene ziliteketezwa," mkazi Innocent Shamvu, anaeleza.

Ni athari inaelezwa tope hilo la moto ilivuka barabara kuu inayounganisha Goma na jiji la Beni, hata kukata misaada muhimu na usambazaji wake.

Hata hivyo, uwanja wa ndege wa jijini Goma unaelezwa haukuguswa, ingawaje kuna madai nao umeathiriwa.

Volkano hiyo inayotoka umbali wa kilomita 10 kutoka Goma, ililipuka mara ya mwisho mwaka 2002 na kuua watu 250, wengine 120,000 walikosa makazi.

**PILIKA ILIKOANZIA**

Kunaelezwa wakazi walianza kuondoka mahali hapo hata kabla serikali haijatangaza mpango wa uokoaji, usiku umati wa watu ulionekana ukikimbia wamebea magodoro na vitu vingine, wakikimbia kwa miguu.

Nchini Rwanda kunaelezwa kuna zaidi ya watu 3,000 walivuka rasmi kutoka Goma, ingawa wengi walianza kurudi makwao DRC baada ya siku chache.

Mkazi wa Goma, Richard Bahati, anasimulia alikuwa nyumbani kwake na ghafla akasikia mayowe na yaliyomtia shaka, huku anga ikionekana kwa rangi nyekundu.

"Niliishi kupitia shida na volkano hii mnamo 2002. Volkano hiyo iliharibu nyumba zetu zote na mali," anaeleza.

Mfanyabiashara, Kambere Ombeni, ni miongoni mwa waliorudi katika eneo la tukio, huku vifusi vikitapakaa kila kona. Ana usemi: "Tulitazama nyumba zote katika eneo la Nyarigongo likichomeka moto. Moto ulifika hadi hapa hata sasa tunaweza kuona uji wa mlipuko wa volcano hiyo."

Mkaazi mwingine, Irene Baula, ana simulizi kwamba watu watahitaji msaada wa serikali, katika kujenga upya maisha yao.

"Kuna ardhi, watu, idadi ambayo imepoteza kila kitu, pengine pia kuna vifo, ni nani anayejua?" anasema.

Tom Costa, kutoka Baraza la Wakimbizi la Norway mjini Goma, anaeleza kilichotokea kwa kauli:"Uji uliokuwa ukitiririka ulikuwa polepole sana kama kilomita kwa saa, lakini haukusita... ulianza kuchoma nyumba."

Anakiri mashirika ya kutetea hali za binadamu yalishaanza ukaguzi wa kuwasadia waathirika.

Mlima Nyiragongo, umo katika milima inayolipuka Volkano, lakini kulikuwa na shaka kwamba, halikukaguliwa kwa kina, na Shirika la Kuchunguza Milipuko ya Volcano mjini Goma, tangu Benki ya Dunia ilipositisha ufadhili, kutokana na madai ya ufisadi.

Profesa Mike Burton, Mtaalamu wa Milipuko ya Volcano katika Chuo Kikuu cha Manchester nchini Uingereza, anasema kwamba uji wa volcano katika mlima Nyiragongo unatiririka kwa kasi kubwa.

Katika ripoti yake, shirika hilo lilitahadharisha kwamba "vitendo vya ardhini vya mlima huo vimeongezeka".

Mwaka uliopita, Mkurugenzi wa shirika hilo mjini Goma, alishatamka kwamba mlima huo wa Volkano, umekuwa ukijaa haraka na kuongezea uwezekano wa mlipuko katika miaka michache ijayo.

Pia, anatahadharisha tetemeko la ardhi linaweza kusababisha janga mapema.

Mlipuko mbaya zaidi wa volkano katika mlima huo ulitokea mwaka 1977 kwa kuua watu 600.

• *Kwa mujibu wa BBC*

# MABADILIKO SEKTA YA MAJI: NYASA WAJIBIWA

Na Mwandishi wetu

Maji ni huduma muhimu katika maisha ya kila siku, hivyo maji ni uhai. Maendeleo yoyote yanahitaji huduma ya maji. Serikali kupitia Wizara ya Maji imeweka kipaumbele katika kuhakikisha huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza inamfikia mwananchi, maeneo ya mijini na vijijini. Wananchi ndio wadau wakuu wa serikali na wizara haitakuwa kikwazo katika kufanikisha huduma ya maji kwa wananchi.

Hatua hizo zinazochukuliwa na serikali zinalenga kuleta maendeleo kwa wananchi na kuwawezesha kutekeleza shughuli za kimaendeleo katika sekta nyingine na kujiongezea kipato.

Sasa wananchi wa vijiji vya Lundo, Lipingo na Ngindo wilayani Nyasa Mkoani Ruvuma wana kila sababu ya kufurahi. Ule mwendo wa kutafuta huduma ya maji unakoma baada ya serikali kufanyia kazi mahitaji yao kuhusu maji.

Wizara ya Maji, imetekeleza mradi wa maji wa pamoja wa vijiji hivyo vitatu. Mradi huo umesimamiwa na Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), ambayo ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Maji.

Mradi huu una thamani ya zaidi ya shilingi milioni mia nne, utahudumia wananchi zaidi ya elfu kumi na nne ambao ni wakazi wa vijiji vya Lundo, Lipingo na Ngido na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2021.

Kukamilika kwa mradi huu kutachochea zaidi kasi ya maendeleo, ikiwamo ya kiuchumi na kuboresha zaidi maeneo ya huduma za umma kama vile afya na shule.

Mkuu wa Wilaya ya Nyasa Bi. Isabela Chillumba anasema mradi huo utaleta mapinduzi makubwa na kuondosha magonjwa ya mlipuko ambayo yanapotokea huwafanya wananchi kukosa utulivu katika utekelezaji wa shughuli za kiuchumi, na kazi nyingine za kuwaletea maendeleo.

"Naishukuru sana serikali na Wizara ya Maji kwa mradi huu ambao upo katika hatua za mwisho za utekelezaji, ni hakika serikali imewajibu wananchi kuhusu huduma ya maji na sasa tutapata utulivu kabisa tofauti na awali ambapo wananchi walihangaika", Mkuu wa Wilaya Nyasa Isabela Chillumba amesema.

Naye Maiko Gidion mnufaika wa mradi huo anasema ukosefu wa maji ulikuwa ni kilio kwa wananchi.

"Tunaishukuru serikali kwa kutupatia mradi huu na kufanikisha ujenzi wa vituo ishirini vya kuchotea maji wananchi katika kijiji chetu cha Lundo", Maiko Gidion anasema na kuongeza kuwa huduma ya maji itawanufaisha katika mambo mengi, ikiwamo muda wa kufanya kazi nyingine za kujiongezea kipato.

Naye, Ernesty Mahay Matumbi mwenyeji wa Ndindo amesema kwa serikali kufanikisha mradi huo ni muda sahihi kwani utasaidia jamii kuibua miradi mingine ambayo lazima itumie huduma za maji.

"Maji haya yatatusaidia kufanya shughuli mbalimbali ikiwamo biashara, ujenzi na masuala mengine ya maendeleo. Tunaomba tushirikiane katika kutunza vyanzo vya maji kwa kuzuia shughuli mbalimbali, ikiwamo ujenzi wa makazi katika vyanzo vya maji. Hatua hii itasaidia mradi wetu kuwa endelevu" Ernesty anasema na kuongeza usimamizi dhabiti wa mradi ni jambo la msingi katika kuhakikisha thamani ya fedha iliyotumika katika ujenzi inawafikia wananchi.



Naibu Waziri wa Maji, Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) akikagua mradi wa maji wa Nyasa, anayetoa maelezo ni Meneja wa RUWASA Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Rebman Ganshonga.



*Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) akijumuika na wataalam wa ufundi katika kuchanganganya udongo wa ujenzi (Zege) katika moja ya mradi wa maji hivi karibuni.*

Kwa upande wake Meneja wa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Nyasa Mhandisi Evaristo Ngole amesema mradi wa pamoja wa Lundo unatekelezwa kwa fedha za Malipo kwa Matokea (P4R) ambapo fedha iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo ni zaidi ya shilingi Milioni 400.

Mhandisi Ngole anasema mradi huo unatekelezwa kwa kuwatumia wataalam wa Wizara ya Maji (kwa utaratibu wa force account). Ametoa pongezi kwa wananchi kwa kushiriki kikamilifu katika kufanikisha mradi huo, kwa kuwa walinzi wa vifaa vya mradi pamoja na miundombinu.

"Wananchi wawe pamoja na sisi. Mradi huu utakamilika kwa wakati katika viwango vilivyokusudiwa, na hakika hapa yanaenda kutokea mabadiliko makubwa kupitia sekta ya maji." Mhandisi Ngole anasema.

Amesema kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa chanzo cha maji kwa ajili ya kijiji cha Lundo na Lipingo, ukarabati wa chanzo cha maji, ujenzi wa vituo 38 vya kuchotea maji wananchi na ujenzi wa mtandao wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa km 24.2.

Utekelezaji wa mradi huu ni moja ya malengo ya Wizara kuhakikisha inawafikishia Watanzania wote huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza kwa haraka. Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) anasema ni mapinduzi ya mabadiliko katika sekta ya maji.

Waziri Aweso anasema kila mtaalam awajibike katika eneo lake ipasavyo, na awashirikishe viongozi na wananchi ili wajue maendeleo ya miradi ya maji na pia kupokea mrejesho wao kuhusu miradi ya maji hapa nchini.

Mhe. Aweso anasema Wizara anayoiongoza haitakuwa kikwazo katika kuhakikisha wananchi katika maeneo mbalimbali hapa nchini wanapata huduma ya majisafi na salama.

Anasema kuwa mpango mkakati wa utendaji wa Wizara ya Maji ni kuhakikisha fedha zote za utekelezaji wa miradi ya maji zinasimamiwa na kutumika ipasavyo na hatamvumilia mkandarasi wala wataalam atakayeonekana kukwamisha juhudi za Serikali za kufikisha huduma ya majisafi, salama na ya kutosheleza kwa wananchi.

Naye Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) akiwa Nyasa amesema baadhi ya miradi ambayo ilikuwa imekwama kwa muda mrefu itakwamuliwa yote ilhali miradi mipya ikiendelea kutekelezwa ili kuhakikisha "mama anatua ndoo ya maji kichwani, na maji yanapatikana bombani" hivyo kutoa fursa kwa wananchi kushiriki kazi nyingine za maendeleo.

Mhe. Mahundi amewataka watalaam kutoa elimu zaidi kuhusu utunzaji wa vyanzo vya maji, na miundo mbinu ya miradi ili kuhakikisha huduma za maji zinawafikia wananchi wengi na kuwa endelevu.

Serikali ya Awamu ya Sita imejipanga kuleta mageuzi makubwa katika Sekta ya Maji kwa lengo la kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji kufikia asilimia 85 vijijini na asilimia 95 mijini ifikapo mwaka 2025.

MAZINGIRA

## WAKATI UJERUMANI IMEWEKEZA BIL. 56...

# Wadau, serikali waingia ubia kutibu tabianchi, vidonda corona hifadhini

## •Kaulimbiu 'kuhimili Mabadiliko Tabianchi'

**Na Maulid Mmbaga**

MABADILIKO ya tabianchi duniani ni ujumla wa magumu ya dunia kupata tafsiri mpya katika maeneo kama mvua na kina cha maji ya bahari, hali inayoangukia mapya kiuchumi, kisiasa na kijamii dhidi ya maendeleo ya umma.

Shirika la Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP) linafanya kazi na vyombo vya kimataifa, kanda, kitaifa na mkoa, kusaidia kukabili mabadiliko, ikihimiza kupunguza uchafuzi wa anga, pia kwingineko kunakohimili hali ya hewa.

Hadi sasa UNDP inasaidia kukabili mabadiliko ya tabianchi nchini, ikisisitiza mikakati ya kukabiliana nayo, pia mapitio ya mpango wa taifa wa marekebisho yake.

Moja ya maeneo inayoshughulikia Serikali ya Zanzibar, pia ya Muungano katika kujumuisha mabadiliko ya tabianchi kwenye mipango ya maendeleo kitaifa, huku ikiimarisha uwezo wa kusimamia mabadiliko ya tabianchi na kupunguza uchafuzi wa anga, ukataji misitu na uharibifu wa ardhi.

Kuna maendeleo mataifa ya kigeni yenye ubalozi nchini yamejitokeza kuisaidia serikali kupambana na mabadiliko ya tabianchi na athari zake, ili kuijengea nchi uchumi stahimilivu.



Mazingira ndani ya Hifadhi ya Taifa Serengeti, ambako kumepata msaada. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**MCHANGO WA EU**

Mkuu wa Jumuiya ya Ulaya (EU), nchini na Afrika Mashariki, Balozi Manfredo Fanti na Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Hamad Chande, siku tisa zilizopita walizindua kampeni ya kupambana na mabadiliko hali ya hewa na athari zake, wakitumia kaulimbiu 'Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi.'

Ni uzinduzi uliofanyika eneo la Posta jijini Dar es Salaam, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ikiwakilishwa na Mkurugenzi wa Masuala ya Diaspora, Balozi Anisa Mbega, pia Mkurugenzi wa Europa na Amerika, wakimwakilisha Katibu Mkuu, Hassan Mwamweta.

Balozi wa Umoja wa Ulaya, Fanti, anasema 'mpango wa kijani' kwao ni fursa inayowafikishia malengo waliokusudia itakapofika mwaka 2050.

Anaeleza: "Marekebisho ya hali ya hewa ni jambo muhimu katika kufanikisha uthabiti zaidi na maisha endelevu kwa kiwango cha kimataifa.

"Tunaweza kuona hii katika miradi yetu nchini Tanzania ambayo inaonyesha kuwa jamii, zinapiga hatua na kuwa na uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa.

"Pia, tunajivunia kutimiza miaka 45 ya ushirikiano na Tanzania. Hii pia ni njia tofauti ya kuadhimisha Mei 9, Siku ya Ulaya, sherehe ambayo itafanyika mara tu hali itakaporuhusu."

**TAHADHARI HATARI**

Balozi Fanti, Tanzania iko hatarini kuathiriwa na mabadiliko ya hali ya hewa, huku idadi kubwa ya wakazi vijijini wanategemea chakula kutoka kilimo cha mvua.

EU inahimiza maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi kwa manufaa ya usalama wa chakula na lishe na Balozi Fanti anasema kinachofanyika sasa ni kushughulikia mipango anuwai.

Anaitaja kuwa dhana inayoanza na sera za maendeleo za wadau wanaounga mkono na kuendeleza michango iliyoamuliwa kitaifa katika miradi ya kijamii kuanzia vijijini.

Makubaliano yalijumuisha: Kukuza njia mpya za kilimo, mifugo, maji, nishatil na usimamizi wa maliasili kwa vijiji vilivyochaguliwa.

Balozi Fanti anadokeza mifano ya utekekezaji inajumuisha kilimo cha mseto, uvunaji maji ya mvua na matumizi ya majiko sahihi.

"EU inafanya kazi zaidi juu ya usimamizi wa maliasili uliotengwa na jamii kwa wanyamapori, misitu na mazingira ya baharini. Msaada umetolewa kwa maendeleo ya maeneo mawili ya usimamizi wa wanyamapori katika hadhi ya Serengeti Magharibi.

"Mengine ni mawili katika maeneo oevu ya Kilombero na Rufiji, usimamizi shirikishi wa misitu katika Mkoa wa Kilimanjaro, Manyara na Morogoro na usimamizi wa ushirikiano wa uvuvi katika ukanda wa Pwani kutoka Dar es Salaam hadi Mtwara," anafafanua.

**DARASA LA SANAA**

Ubalozi wa Uholanzi nchini umeona umuhimu wa kutumika sanaa za picha na video kwa ajili ya kuongeza uelewa wa kinachojiri duniani na uhalisi wa mabadiliko tabianchi.

Katibu wa Uchumi wa Ubalozi huo, Mathijs Eeuwen, anasema walifanya Maonyesho ya Picha 21 na Video nchini, tatu ndizo zilichaguliwa kuwa na ujumbe stahiki unaogusa athari za mazingira.

"Kuona kwa macho kuna tabia ya ushawishi. Picha huzungumza mengi juu ya athari za mabadiliko ya hali ya hewa. Hivyo, wasanii wanajitahidi kutumia kazi yao ya sanaa katika kuongeza uelewa kwa jamii juu ya mabadiliko ya tabianchi," anasema.

Mpigapicha kutoka ubalozi huo, Kader Lohuizen, anasema kuna athari mbaya za mazingira na amekuwa akitumia picha kuonyesha kasi ya joto na athari zake sehemu nyingi duniani.

"Mkataba wa Paris (Mazingira, Desemba 2015) unasema joto halipaswi kuongezeka kwa zaidi ya nyuzi mbili duniani. Ikiwa halijoto haitashuka katika maeneo ya pwani, itasababisha hali ya hewa kuwa mbaya," anasema Kader.



Nchini Indonesia, maji yanaongezeka kina kati ya sentimita 20 na 30 kila mwaka, hata kubomoa kingo, hata kuporomoka za ufukweni, hata mji mkuu kulazimika kuhamishwa.

Bangladesh, nchi hiyo inatajawa kukumbwa na dhoruba, vimbunga na maji bahari kuongezeka kina, hali inayoathiri kilimo ardhini, pia maji ya kunywa yanachafuliwa.

**UNDUGU WA UJERUMANI**

Wizara ya Maliasili na Utalii, inaitaja Ujerumani kuwa mshirika muhimu nchini katika hifadhi za baioanuwai, mzizi mkuu ukianza urafiki uliojengwa na waasisi wa taifa na aliyekuwa mwanzoolojia wake mwandamizi, Prof. Bernhard Grizmek.

Mwaka huu Tanzania na Ujerumani zinasherehekea miaka 60 ya uhusiano huo, zikiwa zimetumia zaidi ya Sh. bilioni 300 (Euro Milioni 106) kwa miaka mitano iliyopita, katika hifadhi asili na wanyamapori nchini.

Katika mwendelezo wake, mwishoni mwa wiki iliyopita kulishuhudiwa ushahidi wa kuingiwa makubaliano mapya yanayohusu mabadiliko ya tabianchi, Ujerumani kufadhili dharura ya Sh. Bilioni 56 (Euro million 20) kwenye mradi wa miaka mitatu wa utalii, kusaidia hifadhi tatu; Serengeti, Nyerere na Selous.

Hiyo ni baada ya Balozi wa Ujerumani nchini, Regine Hess, kutembelea Hifadhi ya Taifa Serengeti, alikoshuhudia athari za janga la corona duniani iliyoathiri utalii na kushusha mapato hifadhini.

**SERIKALI INATAMBUAJE?**

Mkurugenzi wa Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Andrew Komba, anasema mchango wa taasisi hizo ikiwamo Shirika la Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira na Wanyama Pori (WWF), unatambulika na watashirikiana na wadau kuhakikisha kunakuwapo hali ya hewa na mazingira salama.

Komba anasema, ni muda mrefu taasisi hizo zimekuwa zikishirikiana na serikali kuboresha hifadhi ya mimea, masuala ya asili, mabadiliko tabianchi na ustahimilivu wa jamii katika mazingira.

Anaahidi serikali itatoa mchango wa sera, miongozo na vipaumbele stahiki vitakavyowawezesha wadau mazingira kufanya kazi katika mazingira rafiki nchini.

MAZINGIRA

# Mradi 'Safari City' utakavyong'arisha upya mazingira ya jiji la Arusha



Picha ya uhalisia wa mandhari ya Mradi wa Arusha City, unaoliibua upya jiji hilo katika ubora wa ngazi mpya, mkakati unaoandaliwa na Shirika la Nyumba la Taifa. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

**Na Mwandishi Wetu**

JIJI la Arusha linasifika kwa mandhari nzuri, kutokana na kuwa na vivutio mbalimbali vya asili kama vile Mlima Meru, Hifadhi ya Taifa ya Arusha, maporomoko na mito, vyote vikiwa vimezungukwa na uoto wa asili. Mandhari hiyo imekuwa miongoni mwa vivutio vikubwa vya utalii.

Mradi wa kisasa uliobuniwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ujulikanao kama Safari City, sasa unatajwa kuwa matarajio ya kuboresha zaidi mwonekano wa jiji la Arusha na kung'arisha mazingira yake.

Shirika hilo kongwe katika huduma ya nyumba na makazi, linatekeleza mpango huo kabambe ulioandaliwa tangu mwaka 2014 katika eneo la Burka Mateves, lenye ukubwa wa ekari 587.

Hapo, msingi wake ni mahsusi kwa ajili ya uendelezaji nyumba za makazi, majengo ya biashara na huduma mbalimbali za kijamii.

Miongoni mwa huduma hizo za jamii zitakazopamba Safari City ni pamoja na shule, vyuo, hospitali, sehemu za ibada, michezo, maeneo ya mapumziko, na viwanda vidogo vidogo vidogo.

Pia, kunatarajiwa kuwapo maeneo ya kusimamia usalama wa mji, kama vile kituo cha polisi na zimamoto, na maeneo ya wazi ya kupimzikia na hata burudani.

Meneja Habari na Uhusiano wa NHC, Muungano Saguya, anaueleza kuwa ni mradi uliopo umbali wa kiasi cha kilomita 13 kutoka katikati ya jiji la Arusha, na kilomita tatu tu kutoka iliko Uwanja wa Ndege wa Arusha.

Ujumla wake ni mbinu ya kimazingira, inayolenga kulisaidia jiji hilo la kitalii katika endelezaji wa usimamizi madhubuti wa mpango kabambe, kama ulivyoandaliwa.

Saguya anafafanua:"Tunakusudia kuhakikisha kuwa kunakuwepo vitovu vya miji vinavyojitegemea na kufanya miji iwe ya kisasa zaidi, kwa kupangiliwa kwa miundombinu imara."

Anaongeza kuwa mradi huo, pia unalenga kusaidia kupunguza msongamano unaoongezeka kila uchao jijini Arusha na kuwawezesha watu binafsi, kampuni na taasisi mbalimbali kupata maeneo yenye huduma muhimu za kijamii.

Ofisa Habari huyo anaorodhesha upatikanaji kirahisi wa mahitaji hayo ya kijamii kama vile maji, umeme na barabara, kwa uendelezaji wa nyumba za makazi, maofisi, majengo ya huduma mbalimbali na biashara.

Tayari shirika limeshauza jumla ya viwanja 701 tangu mwaka 2016 kwa ajili ya makazi, biashara, maeneo ya ofisi na viwanda vidogo.

"Pia, shirika limeweza kuhifadhi jumla ya viwanja 300 kwa ajili ya kuviendeleza katika siku zijazo. Viwanja vilivyobakia, bado vinaendelea kuuzwa kwa wananchi mbalimbali," anaeleza meneja huyo.

Anataja maboresho mengine ni pamoja na kuitikia maoni ya wadau mbalimbali, sasa NHC imepunguza bei ya viwanja katika eneo la Safari City, kwa kuzingatia hali ya vipato vya watu.

**MAPYA YA KUVUTIA**

Katika punguzo hilo bei ya viwanja ilishuka kwa asilimia 40, akitumia mfano mita moja ya mraba iliyokuwa inauzwa kwa Sh. 35,000, sasa inauzwa kwa beo Sh. 21,000.

Saguya anafafanua kuwa, mteja anapewa fursa ya kulipa kwa awamu ndani ya muda wa miezi 60 (miaka mitano), ambayo kila mwezi anaweza kulipia kiasi cha Sh. 131,000 pasipo na riba yoyote.

Anasema tayari huduma wezeshi zote muhimu kama maji, umeme na barabara zimefikishwa Safari City.

Miundombinu ya barabara nayo inaendelea kutengenezwa na serikali, ili kuwawezesha wananchi walionunua viwanja katika eneo hilo kuyaendeleza maeneo yao na kuwafanya wengine wanaokusudia kununua kuufikia kirahisi mji huo.

Kwa mujibu wa Ofisa Habari huyo, tayari watu binafsi na taasisi mbalimbali za kiserikali zinaendelea na ujenzi katika mji huo, huku wengine wakiwa kwenye maandalizi ya ujenzi.

Miongoni mwa taasisi zinazoendeleza ujenzi katika eneo hilo, ni pamoja na Mamlaka ya MajiSafi na Usafi wa Mazingira Arusha (AUWSA) wanaojenga ofisi ya kanda na Baraza la Taifa la Vyuo vya Ufundi (NACTE), wanaotarajia kuanza ujenzi wa ofisi zao hivi karibuni.

Taasisi nyingine zinazojiandaa kwa ujenzi ni pamoja na Mamlaka ya Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (SUMATRA), Wakala wa Usalama Mahali pa Kazi (OSHA), majeshi ya Zimamoto na Uokoaji, pia Polisi, kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali ya kiserikali kwa wananchi wa jijini Arusha.

Katika utunzaji wa mazingira, NHC imepanda miti mingi katika viwanja vya Safari City, ili kuendana na azma ya serikali ya kuhakikisha wananchi wanaishi katika mazingira bora na salama kwa afya zao.

Katika hatua nyingine, Shirika la Nyumba, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Umilikishaji Ardhi Mkoa wa Arusha tayari limeshawakabidhi wateja 190 hati miliki, ili waweze kuviendeleza viwanja vyao.

"Kwa utaratibu uliowekwa, wateja hawa wanatakiwa kuanza uendelezaji wa viwanja hivyo mapema iwezekanavyo. Hii inasisitizwa, ili kutekeleza madhumuni ya uendelezaji wa mji huu wa Safari City," anafafanua meneja habari na uhusiano.

Shirika hilo lililoanzishwa mara baada ya uhuru kwa lengo la kuendeleza makazi, limewakaribisha wananchi, kampuni, taasisi mbalimbali za serikali na binafsi ndani na nje ya nchi kuwekeza Safari City, ili kuchochea maendeleo mbalimbali ndani ya jiji la Arusha.





# Watumwa ng'ambo kufuatilia vifaa vya bwawa la Nyerere

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

SERIKALI imetuma wataalamu watatu nje ya nchi kuhakiki ubora na ufungwaji wa mitambo itakayofungwa kwenye mradi wa umeme wa bwawa la Nyerere.

Aidha, transfoma sita kati ya 27 za kupooza umeme itakayotumika kwenye mradi huo tayari imewasili nchini.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza kwenye mahojiano ya runinga jijini Dodoma kuhusu maendeleo ya mradi huo.

Alisema wataalamu hao watahakiki mitambo hiyo kulingana na thamani ya fedha na kueleza kuwa ujenzi umefikia asilimia 52.8 na uzalishaji wa umeme utaanza Juni mwakani.

"Hatua madhubuti ambazo tumechukua ni kujihakikishia vifaa vinavyotengenezwa nje vipo na vimefikia hatua gani," alisema.

Aliongeza kuwa wataalamu hao watatu waandamizi wametumwa kwenda kuangalia zoezi la ufungwaji vifaa ili wasiuziwe mbuzi kwenye gunia.

"Maeneo muhimu matano ya ujenzi wa mradi kwasasa ni ujenzi wa bwawa, kituo cha kufua umeme, kituo cha 'kuswitch umeme, pamoja na kingo za kupitisha umeme kutoka kwenye bwawa kwenda kwenye 'power house' yanaendelea vizuri," alisema.

Alisema hatua ya pili ni kufunga mashine na transfoma ambazo zitaendelea kuingia kutoka kwa watengenezaji wa nje ya nchi.

Aidha, alisema ujazwaji wa maji kwenye bwawa hilo utaanza Septemba mwaka huu hadi Aprili 15, mwaka 2022.

"Bwawa letu limeanza kujengwa kingo zile imara kwa ajili ya kuwa na utayari wa kuzalisha maji matarajio yetu kulingana na mpango tuliojiwekea na wataalamu hadi kufikia Septemba 15, mwaka huu bwawa letu tunaanza kujaza maji," alisema.



Askofu Mkuu wa kanisa maalum la watu wenye ulemavu wa kusikia (Viziwi) la Betheli Baptisti Tanzania (KVBBT), Frenk Salungi, akizungumza kwa ishara na washiriki wa warsha ya uhamasishaji na utolewaji wa huduma shirikishi za afya kwa watu wenye ulemavu wa usikivu wakiwamo, madaktari, wazazi na watumishi ngazi ya kata, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Serikali yaombwa madawati na wataalamu kusaidia wenye uziwi

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

KUKOSEKANA kwa madawati na wahudumu wanaofahamu lugha ya mawasiliano ya wenye uziwi hospitalini na vituo vya afya, kumechangia kwa kiasi kikubwa wenye mahitaji kukosa huduma hizo.

Ili kuwasaidia wenye ulemavu huo, serikali imeombwa kuweka madawati maalum ya huduma ya afya kwa watu wenye ulemavu huo wa wakutosikia kwenye hospitali na vituo vya afya ili kusaidia kutoa miongozo ya upatikanaji wa huduma.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Bethel Baptists Deaf Church Tanzania (BBDCT), Frank Sarungi, aliyasema hayo jana kwenye ufunguzi wa mradi wa kuhamasisha utolewaji wa huduma shirikishi za afya kwa watu wenye ulemavu iliyofanyika Dodoma.

Alisema kuwa kukosekana kwa madawati na miongozo imechangia kwa kiasi kikubwa kuwa na mazingira magumu ya upatikanaji wa huduma ya afya kwa watu hao.

Akizungumza kwenye ufunguzi wa mradi huo uliofadhiliwa na Taasisi isiyo ya kiserikali ya The Foundation for Civil Society (FCS), askofu huyo alisema mradi unalenga kukusanya maoni mbalimbali ya namna ya kuboresha huduma za afya kwa wenye ulemavu.

Sarungi alisema kuwa kukosekana kwa mawasiliano kupitia miongozo na madawati ya afya ya watu wenye ulemavu imedidimiza na kuonekana ulemavu ni kama ugonjwa.

"Inasikitisha makundi ya watu wenye ulemavu mkoa wa Dodoma, walio wengi hawajui wajibu wala haki yao ya upatikanaji wa huduma za afya pale wanapoumwa au kupata ajali huwa wanatapatapa hawajui pakuanzia wala pakuishia hii yote ni kutokana na ukosefu wa madawati na miongozo ya namna ya kupata matibabu," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa Muuguzi na Mkunga Mfawidhi Msaidizi, Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Stella Lupembe, alisema kuwa serikali inatambua ugumu wanaokutana nao watu wenye ulemavu wasiosikia katika kupata huduma ya afya zinazotolewa kwenye vituo vya afya, hospitalini na maeneo mengineyo.

"Kuna kila sababu watumishi mbalimbali wakiwamo wa afya kujitokeza kusoma na kuijua lugha ya alama ili kuwahudumia watu wenye ulemavu wasioona kwa kutumia madawati na miongozo," alisema.

Aliwaomba wanafunzi wasiosikia wapende kusoma masomo ya sayansi na mawasiliano ili kuwahudumia jamii hiyo pindi watakapokuwa wahudumu wa afya.

# Mbunge aonya sekta korosho iko taabani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, amesema sekta ya korosho ipo kwenye hatihati kutokana na kutoundwa kwa bodi ya korosho kwa miaka mitatu sasa.

Aidha, ameishauri serikali kurejesha mfuko wa kuendeleza zao ili fedha hizo zitumike ipasavyo na kwamba ili suala hilo lifanikiwe lazima kuwapo na bodi imara.

Akichangia juzi makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo ya mwaka 2021/22, Chikota alisema kilichopo sasa hivi kwenye sekta ya korosho ni kizungumkuti.

"Hii ni kwa sababu bodi haijaundwa kwa miaka mitatu sasa lakini hata mtendaji aliyepo ni kaimu na ile bodi ni 'lidudu' lizito kwa hiyo lazima tupate mtendaji ambaye yupo imara na muda wote atakuwa anashughulikia korosho na pengine hata mzigo uliopo wizarani utapungua kwa sababu mambo mengine watafanya kwenye ngazi ya bodi ya korosho," alisema.

Alifafanua kuwa mfuko huo ulikuwa na muhimu sana kwa sababu ulitoa fedha kwa ajili ya utafiti, wagani katika halmashauri, usimamizi wa halmashauri na uligharamia ubanguaji mpaka usambazaji wa miche iliyosambazwa nchini.

"Fedha tulizitoa lakini zingeachwa kule kwa sasa tungekuwa tunahesabu kuwa tumezalisha tani 5,000,000 lakini zilinyofolewa kabla ya muda wake hivyo kushauri mfuko urejeshwe ili hata mikoa mingine ambayo inalima korosho kwa sasa inufaike na sekta hiyo maana wasipofanya hivyo itakuwa maumivu," alieleza.

Kadhalika, Chikota alisema kuna tatizo kwenye ushirika na kushauri suala hilo liangaliwe kama ni sheria ya ushirika, tume au ofisi ya mrajisi wa ushirika na pia uchunguzwe na kufanyiwa marekebisho makubwa.

"Sasa hivi wizara inataka kufanya mabadiliko ya marekebisho ya sheria inawezekana hata ikibadilishwa bado matatizo yatabaki vilevile hivyo mfumo wa uendeshaji uangaliwe."

"Haiwezekani sheria ya ushirika inasema kwamba mtendaji wa AMCOS kiwango chake cha elimu kisipungue kidato cha nne, lakini anachukuliwa mtendaji ambaye hana kiwango hicho viongozi wengine wapo lakini hakuna hatua inayochukuliwa fedha zikipotea tunaanza kulalamika," alisema.

Kwa upande wake, Mbunge wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu, aliomba serikali kuweka msisitizo katika mambo matatu ili kumsaidia mkulima kupata tija katika kilimo anachofanya na hivyo kuiwezesha sekta ya kilimo kuwa na mchango zaidi katika pato la taifa.

Alisema mambo hayo ni utafiti wa mbegu, kilimo cha umwagiliaji na kupunguzwa kwa masharti katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

Mtaturu alisema kilimo ndio kimebeba uchumi wa nchi kutokana na asilimia 80 ya Watanzania kujishughulisha na shughuli za kilimo.

"Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali, tusipokuwa na mbegu bora hatuwezi kuwa na kilimo chenye tija, wananchi watapoteza muda wao nguvu zao nyingi na hatutaweza kwenda mbele bila ya kuwa na mbegu bora," alisema.





# DC awapa viongozi mbinu kukuza ufaulu

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Reuben Mfune, amewakumbusha wenyeviti wa bodi za shule za sekondari, waratibu elimu na wakuu wa shule hizo, kufanyakazi kwa ushirikiano ili kuongeza ufaulu.

Mfune alitoa kauli hiyo wakati wa kikao cha kujadili namna bora ya kuongeza ufaulu kwa shule za sekondari wilayani humo, alisema licha ya serikali kuendelea kuboresha miundombinu ya elimu, kikwazo kipo kwa watumishi katika kuongeza ufaulu.

Alisema kikao hicho kilijadili mikakati ya namna ya kuongeza ufaulu kwa kutumia mbinu shirikishi baina ya wanafunzi na walimu kwa kushirikiana na wazazi.

"Tumekaa kikao kazi cha kujadili namna bora kuongeza ufaulu miongoni mwa mbinu tunazoona zinafaa ni kuanzisha utaratibu wa wanafunzi kula chakula shuleni, watoto kukaa hosteli na kuanza utaratibu wa masomo ya jioni," alisema Mfune.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Daniel Kamwela, alisema walimu wote watakaokuwa wanafaulisha wanafunzi kwenye masomo wanayofundisha ufaulu wa daraja A na B watakuwa wanapatiwa zawadi kama motisha na ofisi yake.

Alisema licha ya baadhi ya shule za sekondari kutokufanya vizuri serikali inaendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu ambapo hadi sasa kuna sekondari 32 na kati ya hizo nne ni kwa ajili ya wasichana tu.

Mkuu wa Idara ya Elimu, Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Anna Shitindi, alisema wamejipanga kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wote wa shule za sekondari kwa kuhakikisha wanaandaa mitihani ya awali kabla ya mitihani ya taifa.

Alisema wataendelea kuhamasisha wazazi kuchangia chakula shuleni pamoja na kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kwa shule zote kubaini dosari zinazojitokeza.

# Madeni ya walimu yatajwa kuwa tishio kwa elimu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WATUMISHI wa umma hasa walimu kuwa na madeni sugu kunachangia kwa kiasi kikubwa matokeo mabaya ya mitihani na maendeleo duni ya kitaalamu kwa wanafunzi.

Hayo yameelezwa juzi na Kaimu Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Wilbrod Yanga, wakati wa mafunzo ya kupanga bajeti kwa ajili ya watumishi wa mkoa huo, ambayo yaliandaliwa na shirika lisilokuwa la kiserikali la Elimisha.

Alisema madai yamechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza weledi kwa watumishi wa umma wakiwamo walimu, hivyo kushindwa kutimiza wajibu wao kama inavyotakiwa.

Alisema walimu hawana amani, hawafurahii uwepo wao shuleni, wanashindwa kuingia hata darasani kufundisha kwa kuogopa kukamatwa au kudaiwa na wadeni wao.

Aliongeza kuwa ni wakati sasa walimu wakapatiwa elimu ya upangaji bajeti ili kuwanusuru na madeni ambayo yamechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza uwajibikaji.

"Kuna kundi kubwa la walimu wanaodaiwa na limechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza ufaulu kwa watoto, unadhani mwalimu mwenye madeni ataweza kufundisha vizuri, akili yake yote itawaza kukamatwa na namna ya kurudisha hela. Ataishia kuchungulia dirishani kuangalia mdeni wake. Nashauri elimu hii iwakifike walimu ili tuwanusuru na mtego wa madeni," alisema Yanga.

Aidha aliongeza kuwa licha ya baadhi ya walimu kuwa na madeni, lakini wanahitaji elimu ya saikolojia ili kukabiliana na madeni hayo kwa madai kuwa wako baadhi yao ambao wamejiingiza kwenye tabia zisizofaa kwenye jamii ikiwamo unywaji wa pombe kupita kiasi na uvutaji bangi.

Alisema tabia hizo zinatokana na msongo wa mawazo, lakini kukosa washauri wazuri ambao watawasaidia namna ya kujinusuru kwenye mtego wa madeni, vilevile aliongeza kuwa elimu ya upangaji wa bajeti kuanzia ngazi ya familia itawasaidia kuwa na nidhamu ya matumizi ya pesa ili kujiepusha na madeni.

Kwa upande wake, Wilfred Kayombo, ambaye ni Mshauri wa Kilimo mkoani Mbeya, alisema mtindo wa maisha na tamaa zimechangia kwa kiasi kikubwa watu kuwa na madeni.

Alisema mtindo wa maisha ambao unatokana na watu kuacha kuishi maisha yao halisi na kuiga wengine kumechangia kuingia kwenye wimbi la madeni kutokana na mazingira hayo alishauri elimu ya upangaji wa bajeti ambayo

inatolewa na Shirika la Elimisha itasaidia kujitambua na kuwa na nidhamu na fedha yeyote inayopatikana.

Ofisa Maendeleo wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Vincent Msola, aliliomba Shirika la Elimisha kutoa elimu ya upangaji bajeti kwa vikundi vilivyopata mikopo na vinavyorajiwa ili kusaidia fedha zilizotolewa zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa.

Ni muhimu elimu ya bajeti ikatolewa kwa vikundi vya wajasiriamali kwa sababu mtu anapata mkopo, lakini hajui anaenda kufanyia nini hizo fedha badala ya kufanya shughuli za kujiingizia kipato kama alivyoomba kwa halmashauri anakwenda kununua nguo, viatu au kwenda kujichana vyakula vizuri alisema Msola.

Mkurugenzi wa Elimisha, Festo Sikagonamo, alisema kwa kiasi kikubwa wamesaidia kubadilisha maisha ya wananchi husussani wa mikoa ya Mbeya na Songwe

kwa kuwapatia elimu ya upangaji bajeti makundi ya vijana na wanawake.

Alisema makundi hayo yamefanikiwa sasa kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha na wameanza kuona mafanikio baada ya kuanzisha miradi na kuandaa mpango kazi ambao unawaongoza mambo muhimu ya kufanya, aliongeza kuwa wanaendelea kuyafikia makundi mengine ikiwamo watumishi wa umma na taasisi binafsi ili kuhakikisha wananchi wanafurahia maisha na kuondokana na msongo wa mawazo kutokana na madeni.




Mlezi wa Klabu ya Roots na Shoots inayojihusisha na kampeni ya usafi wa mazingira jijini Mbeya ambaye ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Iyela, George Mwagala (kulia), akipokea ndoo za kuhifadhia taka kutoka kwa Mhifadhi Misitu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Eunice Mbilinyi, juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# AMCOS 20 zapigwa jeki mashine za kahawa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

VYAMA 20 vya ushirika vya msingi vya wakulima (AMCOS), kutoka mikoa ya Mbeya, Songwe na Ruvuma vimepatiwa mashine ya kupima unyevu kwenye kahawa, lengo likiwa ni kuongeza ubora wa zao hilo ili kukidhi viwango vya soko la nje na ndani.

Akizungumza juzi wakati wa kukabidhi mashine hizo kwa viongozi wa AMCOS, Mkurugenzi wa Taasisi ya Cafe Afrika, Dafosa Sanga, alisema kuwa lengo ni kuongeza ufanisi na tija katika uzalishaji wa kahawa kwa kuzingatia ubora unaohitajika.

Alisema kiasi cha shilingi milioni 50 kimetumika kwa ajili ya kununua mashine hizo ikiwa ni ahadi na utekelezaji wa kuwasaidia wakulima kuboresha maisha yao kupitia zao hilo.

Mradi wetu wa kuendeleza kahawa kwa wakulima wa nyanda za juu kusini unalenga kuongeza uzalishaji na tija ya zao hilo kwa kutumia mbinu bora za kilimo zinazohimili mabadiliko ya tabia nchi. Kuongeza kipato kutokana na wingi na ubora wa kahawa iliyovunwa, kuchakatwa na kuuzwa kwenye masoko bora ikichagizwa na upatikanaji wa huduma jumuishi za kifedha.

Kwa mwaka 2020/2021 wakulima 6,000 wamefikiwa na elimu ya uzalishaji bora wa kahawa na kwamba lengo ni kuwafikia 24,000 kote nchini hususani kuwapatia elimu ya kilimo bora, upatikanaji wa pembejeo za kilimo sambamba na kukarabati mitambo 20 kwenye AMCOS alisema Sanga.

Meneja mradi wa kuendeleza kahawa Agri- Connect mikoa ya Nyanda za Juu Kusini katika mikoa ya Mbeya, Songwe na Ruvuma, Samora Mnyaonga, alisema matarajio ya mradi huo ambao unafadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Sweden la SIDA na Agricultural Non State Actors Forum (ANSAF) ni kuimarisha vyama 60 vya msingi na kuviwezesha kuwa na vituo vya kutoa na kusambaza pembejeo za kilimo, teknolojia na maarifa.

Sambamba na hilo pia kuwezesha utaalamu wa kilimo bora cha kahawa kwa maofisa ugani wa serikali na wadau wengine, wanaoshughulikia sera na mipango kwa kuwapa mafunzo ya kilimo endelevu na matumizi bora ya ardhi.

Aliongeza kuwa watawafikia na kuwawezesha wadau wengine katika mnyororo wa thamani wa kahawa ili kuboresha ufanisi kwenye sekta ya kahawa.

Meneja wa Tanzania Coffee Research Institute (TaCRI), Isaac Mushi, akizungumzia suala hilo alisema, wanaendelea kuwasaidia wakulima kwa kuhakikisha wanafanya utafiti na kutoa ushauri juu ya matumizi sahihi ya udongo ili kuongeza rutuba na mavuno mengi.

Alisema kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo kutasaidia

kuchangia maendeleo jumuishi na endelevu kwenye mnyororo wa thamani wa kahawa ili kuboresha kipato na lishe kwa wakulima wadogo wa mikoa inayotekeleza miradi.





# Wajumbe wataka msitu upewe hadhi kimataifa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wameitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuutangaza misitu wa Jozani (Unguja) na Ngezi (Pemba) kuwa hifadhi ya kimataifa.

Baraza hilo linaamini hatua hiyo itasaidia kuimarisha sekta ya utalii na kuingiza mapato.

Wajumbe wa baraza hilo walitaka kuchukuliwa kwa hatua hiyo juzi walipochangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka ujao wa fedha.

Mwakilishi wa Chaani, Nadir Abdulatif, alisema kuwa kwa zaidi ya miaka 20 serikali imeutangaza Msitu wa Jozani kuwa hifadhi ya kimataifa katika gazeti la serikali, lakini hakuna juhudi zinazoonyesha msitu huo upo kimataifa.

Aliwataka watendaji wa hifadhi ya msitu huo kutengeneza mazingira ya njia zilizopo katika hifadhi hiyo kupitika vizuri ili kuvutia watalii.

Pia alitaka kuimarishwa kwa vivutio vilivyomo katika msitu huo ikiwamo wanyama aina ya kima punju, akisisitiza wanaonekana kupungua.

"Mimi binafsi sijaridhishwa na juhudi za serikali za kuufanya Msitu wa Jozani kuwa hifadhi ya kitaifa kwa sababu zipo kasoro nyingi ambazo tunatakiwa kuzifanyia kazi katika kufikia malengo ya msitu wa hifadhi ya kimataifa," alisema.

Mwakilishi wa Chakechake, Hassan Kaduwara, aliitaka wizara kuimarisha Msitu wa Hifadhi ya Ngezi, Pemba ili kufikia vigezo vya kimataifa na kuwawezesha watalii wanaofika Pemba kutembelea eneo hilo.

Alisema zipo juhudi zimefanywa katika kuimarisha msitu huo ikiwamo kujenga ofisi kwa ajili ya wafanyakazi wa hifadhi hiyo lakini juhudi zaidi zinahitajika.

"Nilitembelea msitu huo na kubaini tunahitaji kufanya kazi ya ziada katika kuimarisha na kuutangaza msitu huo kwa wageni wanaotembelea nchini kwa lengo la kufikia vigezo vya kimataifa," alisema.

Mwakilishi wa Viti Maalum Wanawake Mkoa wa Kaskazini Unguja, Panya Ali Abdalla, aliitaka wizara hiyo kuyatambua maeneo ya vivutio ikiwamo msitu wa Kiwengwa ili kuongeza mapato ya wizara.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdula, akizungumza na uongozi wa Chama cha Skauti Tanzania pamoja na uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ofisini kwake Vuga mjini Zanzibar jana. **PICHA: OMPR – ZNZ**

# Waziri atamba Zanzibar kung'ara uzalishaji viungo

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Dk. Soud Nahoda, amesema serikali imejipanga kurudisha hadhi ya Zanzibar kuwa visiwa vinavyoongoza katika uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa za mazao ya viungo.

Amesema hatua hiyo itawasaidia wakulima kunufaika zaidi na kilimo hicho na kukuza uchumi wa nchi. Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 202/22.

Dk. Nahoda alisema kipaumbele cha wizara katika mwaka wa fedha ni kuimarisha mazao ya viungo kwa wakulima kwa kushirikiana na asasi mbalimbali, hatua ambayo itawawezesha wakulima kupiga hatua kubwa ya kukuza kipato.

Alisema wizara imechukua hatua hiyo baada ya kubaini bei ya mazao ya viungo katika soko la dunia ni nzuri na yenye tija kwa wakulima.

Waziri huyo alisema kuwa katika miaka ya 1960, Zanzibar ilikuwa ikiongoza katika ukanda wa Afrika ya Mashariki kuzalisha mazao ya viungo na kusafirisha katika bara la Asia.

Aliyataja mazao ya viungo ambayo yatapewa kipaumbele katika mwaka wa fedha 2012/22 ni vanila, pilipili manga, pilipili hoho, uzile na mdalasini.

''Kwa mwaka wa fedha 2012/22, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipanga vizuri kuhakikisha mazao ya viungo ya vanila, uzile, pilipili manga na pilipili hoho ambapo tumebaini kwamba bei yake ni nzuri katika soko la dunia na kuwa mkombozi kwa wakulima," alisema. Waziri alisema wizara inaendelea na mikakati yake ya kuimarisha mazao ya nazi pamoja na karafuu ambapo jumla ya miche 500,000 ya mikarafuu itagaiwa bure kwa wakulima.

Alisema miche 500,000 ya minazi mirefu ya Kiafrika itagaiwa kwa wakulima Unguja na Pemba ili kusaidia upatikanaji wa nazi visiwani humo.

"Tumejipanga vizuri kuhakikisha Zanzibar inarudisha hadhi yake ya uzalishaji wa nazi katika Bara la Afrika na kupata mbata inayozalisha mafuta," alisema.

Dk. Nahoda aliliomba Baraza la Wawakilishi kuidhinisha Sh. bilioni 53.7 kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka ujao wa fedha.

Kati yake, Sh. milioni 423 ni kwa ajili ya mradi wa kupambana na wadudu waharibifu wa mazao na matunda, wakiwamo nzi.

# Makamu wa Rais awapa jukumu skauti uzalendo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar ameutaka uongozi wa Chama cha Skauti Tanzania kuwafunda vijana uzalendo ili kuwajengea maadili mema kupiga vita vitendo viovu.

Hemed Suleiman Abdulla alitoa agizo hilo juzi alipokutana kwa mazungumzo na uongozi wa chama hicho uliomtembelea ofisini kwake Vuga, Zanzibar.

Alisema mafunzo ya skauti ni eneo muhimu kwa maslahi ya taifa kutokana na mchango wake mkubwa katika kuwajengea maadili mema vijana sambamba na kuwapatia elimu ya ubunifu.

Alisema kuna haja kwa uongozi wa Skauti Tanzania kuwafunza vijana namna bora ya kutambua ubaya na kupinga rushwa, ubadhirifu na uhujumu uchumi.

Makamu wa Rais aliuhakikishia uongozi huo kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itatoa ushirikiano kwao katika kuhakikisha mchango wa chama hicho unatambulika nchini.

"Jamii lazima itambue kwamba kazi ya kuwalea vijana si ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na chama hiki pekee, bali ni jukumu la jamii kwa ujumla," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho ambaye ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohamed Said, alisema wizara anayoisimamia itahakikisha inaupa ushirikiano uongozi wa Skauti Tanzania ili kusimamia utendaji kwa vijana wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Simai alisema Chama cha Skauti kwa upande wa Zanzibar kimeimarika vyema katika kusaidia malezi bora katika jamii.

Akitoa taarifa kwa Makamu wa Pili wa Rais, Mkuu wa Chama cha Skauti Tanzania, Mwantum Mahiza, alisema chama hicho kwa upande wa Zanzibar kina zaidi ya miaka 109 tangu kuanzishwa kwake na kimekuwa kikipata ushirikiano mzuri kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar.

Kiongozi huyo alisema hivi sasa uongozi wa Skauti unajenga kambi ya kimataifa Makao Makuu ya Nchi jijini Dodoma, hivyo alitumia fursa hiyo kuiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwapatia eneo maalum kwa ajili ya kujenga chuo cha kutolea mafunzo kwa vijana.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

## KUPOTEA KWA PASIPOTI



**RAPHAEL PEACE KAJUBILI** anatangaza kupotelewa na pasipoti ya kusafiria yenye namba za usajili **TAE 140649** iliyotolewa na wizara ya mambo ya ndani ya nchiV( UHAMIAJI ) DAR ES SALAAM mwaka 2019, yoyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/KIJ/RB/264099/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ROBINSON FARLES KIDEDE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 538 AMX** – SUZUKI ESCUDO. CHASSIS NAMBA **TDOIW216908.** ENGINE **NAMBA 206677.** PIA AMEPOTELEWA NA KADI YA NHIF. YEYOTE ATAKAYEZIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/TAB/RB/214400/2021.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

NDUGU **SARAH ARAM MWIPOPO** AMEPOTEZA KADI YAKE YA GARI AINA YA PASSO YENYE USAJILI NAMBA **T 931 DQC** KWA YEYOTE ATAKAE ONA AU KUOKOTA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

**RB NA.DSM/PHQ/RB/81515/2021.**

---

**Katika makama ya mwanzo ya**
**MALIKUNGU (W) MASWA**
**Usimamizi wa mirathi**
**Na 7 2021**
**Ombi la SELEMANI A ROMORE kuteuliwa usimamizi wa mirathi ya marehemu ISSA RAMADHANI KILIMA WA BIAFRA B MASWA KWA.yeyote**

**ANAYEHUSIKA POPOTE PALE ALIPO**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe **02/06/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamii wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU MASWA
HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU

---

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM AT KISUTU**
**CIVIL CASE NO.147 OF 2020**
**WINRAY COMMODITIES LIMITED............PLAINTIFF**
**VERSUS**
**BAJWA FARMERS AND TRADERS LIMITED.........DEFENDANT**
**NOTICE OF DATE OF EXPART JUDGEMENT**

TAKE NOTICE that,the above mentioned case has been fixed for exparte judgement on the 24th day of june 2021,at 1.00pm before Hon. Kassian-PRM
Please be informed
GIVEN under my hand the SEAL of the court this 19th day of May 2021.

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.156/2021**

Ombi la **SIMON BOB MASOY** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **FLORA GABRIEL MASOY**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **25/06/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 25/05/2021**

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Yusuph Asagwile Mwaisunga** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 445 DQF.** Chassis namba **KJ10002685** na Engine namba **MR20547400A.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi Taarifa **MBE/MBE/RB/ 265428/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JAWAD DAWOOD ABDUL KADIR** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba ya usajili **T 472 DRH.** TOYOTA LAND CRUISER. CHASSIS NO. **jeib71j700011831.** ENGINE **NO. ih20184214.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo Cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/265179/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

DICKSON CASSIAN MBANO ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T **632 AXR – SUZUKI SAMURAI. CHASSIS NAMBA SJ70-304133.** ENGINE NAMBA 16197. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **SO/RB/2021.**

***NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA***

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MAYENGA MARKET SUPPLY** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba ya usajili **T845 CAH**
ENGINE NO **6D171124871.**
CHASIS NO **FK629H532056.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
***TAARIFA YA POLISI***
**AR/ARU/RB/185662/2021.**

## ENEO LILILOKO MZAMBARAUNI KATA YA CHAMAZI WILAYA YA TEMEKE LINAUZWA.

TAYARI ENEO LIMEZUNGUSHIWA UZIO WA UKUTA.
NDANI MNA NYUMBA YA KAWAIDA NA MABANDA MATATU,
**PIA KUNA HUDUMA ZA MAJI NA UMEME.**

**KWA MAWASILIANO PIGA SIMU NAMBA 0772 645207 HASSAN AU 0784 694903 ABDULLAH**

**Katika makama ya mwanzo ya**
**MALIKUNGU (W) MASWA**
**Usimamizi wa mirathi**
**Na 7 2021**
**Ombi la SELEMANI A ROMORE kuteuliwa usimamizi wa mirathi ya marehemu ISSA RAMADHANI KILIMA WA BIAFRA B MASWA KWA.yeyote**

**ANAYEHUSIKA POPOTE PALE ALIPO**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe **02/06/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamii wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU MASWA
HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU

**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industial Area,**
**Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## ECOWAS yakutana na viongozi wa Mali wanaoshikiliwa na jeshi

**Bamako,** MALI

WAPATANISHI wa Afrika Magharibi, wamekutana na viongozi wa serikali ya mpito ya Mali ambao wanashikiliwa, siku mbili baada ya viongozi hao kuondolewa madarakani na jeshi.

Rais Bah Ndaw na Waziri Mkuu, Moctar Ouane walikutana na ujumbe wa upatanishi wa Jumuiya ya Uchumi ya nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS), uliowasili jana, kwenye mji mkuu wa Mali, Bamako.

Kiongozi wa jeshi, Kanali Assimi Goita, aliyewaondoa madarakani viongozi hao, ambao walipewa jukumu la kuiongoza serikali ya mpito iliyowekwa Agosti mwaka jana, kuhakikisha kurejea kwa utawala wa kiraia baada ya mapinduzi, alisema ujumbe wa ECOWAS umeruhusiwa kukutana na kufanya mazungumzo na Ndaw na Ouane.

Kiongozi wa ujumbe huo, Rais wa zamani wa Nigeria, Goodluck Jonathan, alisema wapo Bamako kuwasaidia ndugu zao wa Mali, kupata suluhisho la mzozo huo, ingawa ni wazi ECOWAS inaweza kuiwekea vikwazo katika mkutano ujao wa kilele.

"Kwa kweli tuko hapa sababu kuna masuala kadhaa ambayo ECOWAS ina wasiwasi nayo kidogo na kama timu inayopatanisha tunahitaji kuja kuwasikiliza watu wetu.

"Hatuwezi kusema chochote hadi tutakapofanya mazungumzo na vyama vya kiraia, wananchi wa Mali, jeshi na wale waliokuwapo kwenye serikali.

"Baada ya mazungumzo haya basi tutakuwa na kitu cha uhakika cha kuvieleza vyombo vya habari," alifafanua Jonathan.

Juzi, Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU), ECOWAS, Umoja wa Ulaya (EU) na Marekani zilitoa taarifa ya pamoja, kulaani kitendo hicho na kutoa wito kwa viongozi hao kuachiwa mara moja bila masharti yoyote yale.

Ofisa wa ngazi ya juu wa Mali ambaye hakutaka kutajwa jina lake, alisema Ndaw na Ouane, wamepelekwa katika kambi ya kijeshi ya Kati, karibu na Bamako na kwamba wanaendelea vizuri.

Alisema viongozi hao walilala sehemu nzuri pia Rais Ndaw, aliruhusiwa kuonana na daktari wake.

Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, lilifanya mkutano wa dharura wa faragha kuijadili Mali.

Mkutano huo ulipendekezwa na Ufaransa, Niger, Tunisia, Kenya pamoja na Saint Vincent na Grenadines.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Ufaransa, Jean-Yves Le Drian alitangaza awali mjini Paris kwamba, ombi la kufanyika kikao maalum cha baraza hilo, lilipelekwa baada ya mapinduzi kutokea Mali.

Hata hivyo, hakuna dalili kuhusu uwezekano wa kupitishwa kwa tamko la pamoja katika mkutano huo wa dharura.

Katika hatua nyingine, China imezitaka pande zinazohasimiana Mali kumaliza tofauti zao, kupitia njia ya mazungumzo ili kudumisha utulivu na umoja wa kitaifa.

**DW**

# Zuma akana mashtaka dhidi ya ufisadi

**Pietermaritzburg,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa zamani wa Afrika Kusini, Jacob Zuma, amekana mashtaka ya ufisadi katika kesi yake dhidi ya ufisadi mbele ya mahakama ya Pietermaritzburg.

Akionekana mdhaifu na kuongea kwa utulivu jana, kwenye Mahakama hiyo iliyopo mji wa Pietermaritzburg, Jacob Zuma alisema anapinga makosa yote 18 ya ulaghai, ufisadi, ulaghai, ukwepaji wa kodi na utakatishaji fedha haramu.

Mashtaka hayo yanahusiana na matukio ya zaidi ya miongo miwili katika siku za mwanzo za demokrasia ya Afrika Kusini pamoja na mpango mkubwa wa silaha wenye utata.

Zuma na washirika wake wanasisitiza kuwa kesi hiyo ni ya kisiasa.

Umati wa watu ulikusanyika nje ya ukumbi wa mahakama huko mjini Pietermaritzburg, kuashiria kuwa Zuma bado ana umaarufu miongoni mwa wafuasi wake.

Ingawa upo ushahidi mkubwa wa ufisadi uliofanikiwa katika kipindi cha uongozi wa madarakani na Waafrika Kusini wengi wanataka kuona haki ikitendeka.

Zuma, pia anakabiliwa na madai mapya ya ufisadi na huenda akafungwa jela kwa kukiuka amri ya mahakama katika kesi nyingine tofauti.

Waafrika Kusini wanaamini kesi hiyo inaweza kuashiria mabadiliko ya nchi hiyo.

Baadhi ya mashujaa wa ukombozi wa Afrika Kusini waliohai, wamemshtumu Zuma na kumlinganisha na jambazi na kuonya kwamba, itachukua muda mrefu kurekebisha uharibifu alioufanya dhidi ya taasisi changa za nchi.

**BBC**



Rais wa zamani wa Afrika Kusini, Jacob Zuma, akiwasili katika Mahakama Kuu ya Pietermaritzburg, jana, kujibu mashtaka yanayomkabili ikiwamo rushwa. **PICHA: AP**

# UNICEF: Ukosefu wa maji huathiri zaidi watoto

**New York,** MAREKANI

RIPOTI ya Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Watoto (UNICEF), imesema, maeneo yenye machafuko ya Mashariki ya Kati, Afrika, Asia na Ulaya yana uhaba mkubwa wa maji ambao huathiti zaidi watoto.

UNICEF katika ripoti iliyotoa jana, jijini New York, ilisema maeneo hayo yana takribani watu milioni 48 wakiwamo watoto, kuliko na shida kuu ya maji.

Aidha, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, limetaka nchi wanachama kuchukua hatua kali kwa watakaokiuka na kushambulia vyanzo vya maji.

Ilisema ukosefu wa majisafi na salama unaweza kuua watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano mara 20 zaidi kuliko mabomu na risasi katika maeneo ya kivita.

Taarifa ilisema kuna uhitaji mkubwa wa huduma ya majisafi na salama pamoja na miundombinu ya majitaka, kwenye maeneo hayo.

Mapigano na mizozo katika maeneo ya Mashariki ya Kati, Afrika, Asia na Ulaya yanawaweka watoto katika uwezekano wa kufa kutokana na kukosa maji na kisha kupata magonjwa ya kuhara.

Ripoti hiyo ilisema watoto walio dhaifu sana, wapo katika hatari mara nane zaidi kufariki dunia kama watakosa majisafi na salama, ikilinganishwa na waliozaliwa katika mazingira ambayo maji yanapatikana.

Msemaji wa UNICEF Programu za Dharura, Manuel Fontaine alisema: Upatikanaji wa majisafi na salama ni njia ya kuimarisha uhai na haitakiwi kamwe kutumika kama mbinu ya kivita.

"Kushambulia vyanzo vya maji ni kushambulia watoto."

Manuel alisema watoto wanaweza kupoteza maisha akisema, iwapo usambazaji wa maji utasimama, na kwamba magonjwa kama kipindupindu, kuhara yana madhara makubwa.

"Hospitali zinashindwa kufanya kazi na ongezeko la utapiamlo na uchafu huongezeka. Watoto na familia zao mara nyingi hulazimika kutoka nje kwenda kutafuta maji na huko hujiweka kwenye hatari zaidi, hususani wasichana ambao wanaweza kudhurika na vilevile kukumbwa na vitendo vya kiudhalilishaji."

Ripoti ilisema Yemen watu milioni 15.4 hawana maji.

**UN**

## Marekani kuikarabati Gaza

**Gaza,** PALESTINA

MAREKANI imeahidi kuimarisha uhusiano wake na Mamlaka ya Palestina kwa kufungua tena ubalozi wake mdogo, Mashariki mwa Jerusalem na kusaidia katika ujenzi wa ukanda wa Gaza, baada ya mashambulizi ya Jeshi la Israel.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Anthony Blinken, alisema hayo baada ya kukutana na viongozi wa Palestina, huku akimhakikishia Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu kuwa, Marekani inaunga mkono masuala ya usalama.

Waziri huyo wa Marekani, alisema anatambua ugumu wa kurejesha hali ya kuaminiana kati ya Waisrael na Wapalestina, baada ya mzozo wa wiki iliyopita.

Blinken alifanya mazunguzo na Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu na pia Waziri wa Mambo ya Nje, Gabi Ashkenazi na ameahidi kuwa Marekani itatoa mchango mkubwa katika kuukarabati Ukanda wa Gaza.

**RFI**



# GATTUSO

## ASAINI MIAKA MIWILI FIORENTINA

**FLORENCE, Italia**

GENNARO Gattuso atakuwa kocha mpya wa Fiorentina kwa msimu ujao, makubaliano hayo yamefikiwa siku mbili tu baada ya kufukuzwa kule Napoli.

Muda mfupi baada ya Jumapili kutoka sare ya 1-1 na Hellas Verona katika dimba la Diego Armando Maradona na Napoli kumaliza nafasi ya tano kwenye Serie A, rais wake, Aurelio De Laurentiis akathibitisha kumfukuza Gattuso.

Napoli walikwenda kwenye mchezo huo wa mwisho wa ligi ikiwa nafasi ya nne katika msimamo, lakini wakapitwa na Juventus, ambao walipata ushindi wa 4-1 dhidi ya Bologna.

Mkataba wa Gattuso ulikuwa unamalizika mwishoni mwa msimu huu 2020-21 na kushindwa kwa Napoli kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, kumegharimu kibarua chake.

Alishinda mechi 46 kati ya 81 akiwa kocha wa Napoli, akiwa amepata asilimia 56.8 ya ushindi mzuri zaidi kuliko Rafael Benitez (asilimia 52.7) na Carlo Ancelotti (asilimia 52.1), lakini mbaya zaidi kama Ottavio Bianchi (asilimia 56.9) na Maurizio Sarri (asilimia 66.2).

Kiungo huyo wa zamani wa Italia sasa amechukua mikoba ya kuinoa Fiorentina, ambaye waliripotiwa kumwania kwa miezi kadhaa na amechukua mikoba ya Giuseppe Iachini.

## BUFFON KUAMUA MAJALIWA YAKE JUNI

**TURIN, Italia**


GIANLUIGI Buffon bado hajafikiria majaliwa yake baada ya kuondoka Juventus, akibainisha kwamba, hatafanya uamuzi hadi ikifika Juni, mwaka huu.

Kipa huyo mwenye umri wa miaka 43, ambaye amecheza mechi 176 kwa timu ya Taifa ya Italia, kati ya mwaka 1997 na 2018, hivi karibuni alitangaza uamuzi wa kuondoka hapo Bianconeri lakini bado hajajua wapi atakapokwenda kucheza au kustaafu soka.

Buffon alijiunga tena na Juve miaka miwili iliyopita baada ya kukaa msimu wa 2018-19 kule Paris Saint-Germain, lakini kipindi cha pili alikuwa kipa namba mbili mbele ya Wojciech Szczesny.

Alicheza kwa mara ya mwisho katika klabu hiyo mwezi uliopita kwenye fainali ya Coppa Italia wakati Juve ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Atalanta.

Tangu alipojiunga na Juventus akitokea Parma mwaka 2001, Buffon ameshinda mataji 10 ya Serie A na amechezea timu hiyo mechi 657 nyingi zaidi kuliko mchezaji yoyote katika klabu hiyo.




Lakini amesema bado hajajua wapi atakuwa baada ya msimu wa 2021-22 na ataamua mwezi ujao.

"Nimeamua kupumzika kwa siku 15," alisema akiiambia Canale 5.

"Nitafikiria kwa makini kuhusu nini cha kufanya na sijaamua kama nitastaafu au kuendelea kucheza.

"Sina haraka kwa sababu mimi ni mtu wa kawaida na mtulivu, nitaamua tu na mambo yatakuwa sawa muda si mrefu."

# KOEMAN MAMBO BADO MAGUMU

**BARCELONA, Hispania**

RONALD Koeman alikutana na Rais wa Barcelona, Joan Laporta, Jumanne jioni, lakini kwa mujibu wa ripoti majaliwa yake bado hayajajulikana.

Raia huyo wa Uholanzi, Koeman aliiongoza Barca kumaliza nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Hispania msimu huu, ikiwa ni mara ya kwanza kuwa nje ya mbili bora tangu msimu wa 2007-08.

Ingawa aliwaongoza kushinda taji la Copa del Rey.

Walibebwa kwa kiwango kikubwa na Lionel Messi, ambaye alifunga mabao 30 kwenye LaLiga na kushinda taji la nane la Pichichi (mfungaji bora wa ligi), ingawa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 majaliwa yake nayo bado hayajajulikana wakati mkataba wake ukiwa unamalizika mwezi ujao.

Laporta alichukua nafasi ya rais wa zamani, Josep Maria Bartomeu Machi, mwaka huu akirudi kwa mara ya pili hapo Camp Nou.

Koeman aliteuliwa na Bartomeu mwaka jana, baada ya Quique Setien kufukuzwa, huku kocha huyo akisaini mkataba wa miaka miwili.

Ripoti zinasema kwamba Laporta bado majaliwa yake hayajulikani na Jumanne Koeman alikutana na rais wa Barca.

Hata hivyo, gazeti la Marca limeripoti kuwa bado kuna uwezekano wa wawili hao kukutana tena.





# MODRIC:

## NAJISIKIA FAHARI KUCHEZA MADRID

**MADRID, Hispania**

LUKA Modric amesema hakuna hisia kubwa zaidi ya kuichezea Real Madrid baada ya kusaini mkataba mpya wa kuendelea kuwatumikia miamba hao wa LaLiga.

Madrid ilithibitisha Jumanne kwamba, nyota huyo wa kimataifa wa Croatia ambaye angekuwa mchezaji huru mwezi ujao, ameongeza mkataba wa miezi 12.

Hiyo itamfanya mshindi huyo wa Ballon d'Or mwaka 2018 kuwa amekaa hapo kwa muda wa mwongo mmoja hapo Santiago Bernabeu, akiwa amewasili hapo Tottenham kwa euro milioni 35 Agosti, mwaka 2012.

Alishinda mataji 16 wakati wa kipindi chake cha kucheza hapo, yakiwamo mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa mchezaji wa Madrid na sasa akiwa na umri wa miaka 35.

Modric ameripotiwa kukubali kubakia kwa kupunguziwa mshahara wake ili aendelee kucheza Los Blancos.

"Nina furaha kubwa na najisikia fahari kuendelea kucheza kwa mwaka mmoja zaidi," alisema akiiambia Real Madrid TV.

"Hakuna kitu bora zaidi ya kuichezea Real Madrid na hakuna hisia nzuri zaidi kama kucheza hapa Bernabeu."

# URAFIKI KUWAUNGANISHA AGUERO, MESSI BARCA

**BUENES AIRES, Argentina**

MKURUGENZI wa Michezo wa Timu ya Taifa ya Argentina, Hugo Tocalli amezidisha uvumi unaomuunganisha Sergio Aguero na Barcelona, baada ya kuelezea uhusiano wake wa karibu na Lionel Messi.

Tocalli alifanya kazi na wachezaji hao wakati akiwa kocha wa timu ya taifa ya vijana ya Argentina kati ya 2005 na 2007 na kupendekeza kwamba uhusiano wao wa karibu kutoka wakati huo unaweza kuendelea huko Camp Nou.

"Wamekuwa na uhusiano mzuri sana kwa miaka mingi, kila wakati wako pamoja kwenye mikutano ya timu, wamekuwa marafiki tangu wakiwa watoto," alisema Tocalli akiiambia Que t'hi jugues.

"Sasa Leo Messi anaweza kumsaidia Aguero huko Barcelona."

Mkataba wa kumpeleka Aguero Camp Nou umekubaliwa, ingawa bado haujafanywa rasmi na ilithibitishwa na Pep Guardiola katika mahojiano yake baada ya Manchester City kutwaa taji la Ligi Kuu England Jumapili iliyopita.

Guardiola aliendelea kufunguka kuwa atakuwa akicheza pamoja na Messi, nahodha wa Barcelona ambaye bado hajasaini mkataba mpya wa kumbakisha klabuni zaidi ya msimu wa joto.

Aguero atajiunga na Barcelona na mshambuliaji wa Uholanzi Memphis Depay, ambaye atahamia Blaugrana baada ya mkataba wake kumalizika huko Lyon.




# DONNARUMMA AWAAGA WACHEZAJI MILAN

**MILAN, Italia**

GOLIKIPA wa AC Milan, Donnarumma anaripotiwa tayari ameshawaaga wachezaji wenzake baada ya ushindi wa Atalanta dhidi ya Inter Milan, Jumapili iliyopita.

Tuttorsport waliripoti wakala wake, Mino Raiola hajafurahishwa na ofa ya Milan kwa golikipa huyo yenye thamani ya euro milioni nane kwa mwaka, na yeye alitaka mteja wake kulipwa angalau euro milioni 10 kwa mwaka.

Mkataba wa golikipa huyo raia wa Italia unafika mwisho Juni 30, 2021.

Na taarifa zinasema Raiola aliomba mshahara wa kati ya euro milioni 15 na euro milioni 20.

Hata hivyo, Milan wanaonekana kutokuwa na mpango kabisa wa kukubaliana na Raiola, na wanahisi watakuwa wanamnunua mchezaji ambaye wamechangia kumkuza vyema kwenye soka kwa gharama zaidi.

Taarifa kutoka Milan, ziripoti kuwa Donnarumma tayari alikuwa amewaaga marafiki zake na wanatimu wenzie kuwa anaondoka klabuni hapo licha ya klabu yake hii kufuzu Ligi ya Mabingwa kwa msimu ujao.

Kutokana na hali ya mkataba wake na sintofahamu inayoendelea katika makubaliano kati ya wakala wa mchezaji huyu na klabu yake, huenda akashindwa kusalia Milan.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TOTTENHAM YAFIKIRIA KUMREJESHA POCHETTINO

●●● Inaelezwa jina la kocha huyo wa PSG linaongoza katika orodha ya walimu wanaotarajiwa kurithi...

**PARIS,** Ufaransa

GAZETI la Sun limeripoti kuwa Mwenyekiti wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy, atafikiria kumshawishi kocha wake wa zamani, Mauricio Pochettino kurudi klabuni hapo.

Tottenham imekuwa ikihusishwa na majina makubwa wakati wakitafuta kocha mpya wa kuiongoza timu hiyo kwa ajili ya msimu ujao.

**Spurs walimfukuza Jose Mourinho mwezi uliopita na wamemaliza msimu wakiwa nje ya nne bora kwenye Ligi Kuu England, pamoja na kuondolewa kwenye Ligi ya Europa na Dinamo Zagreb, licha ya kuongoza kwa 2-0 katika mchezo wa kwanza.**

Huku uvumi ukiendelea kuvuma kuhusu majaliwa ya mshambuliaji, Harry Kane kutaka kuondoka klabuni hapo, Spurs wanataka kufanya biashara kubwa kwenye dirisha la usajili la majira ya joto.

Pochettino, ambaye aliipeleka Spurs kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2019, kwa sasa anainoa Paris Saint-Germain, ambayo imemaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1.

Gazeti hilo la Sun limedai kuwa Pochettino hana furaha hapo jijini Paris na atafikiria kurudi London, ambako alifukuzwa Novemba, 2019 baada ya matokeo mabaya.

Sky Sports pia limeripoti kwamba, Spurs wapo kwenye mazungumzo na kocha wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Roberto Martinez.

## KWA UFUPI

### SPURS YAMTAKA MARTINEZ

KLABU ya Tottenham Hotspur ipo kwenye mazungumzo na Kocha Mkuu wa Ubelgiji, Roberto Martinez mwenye umri wa miaa 47, wakati harakati za kumsaka atakayechukua nafasi ya Jose Mourinho zikiendelea. (***Sky Sports***)

### WOLVES KUMUUZA NEVES

WOLVES wamejiandaa kumuuza kiungo wao, Ruben Neves (24), kwa dau la pauni milioni 35 ili kupata fedha za kukijenga kikosi chao kwa ajili ya kocha yeyote atakayechukua nafasi hiyo baada ya kuondoka kwa Nuno Espirito Santo. (***The Athletic - subscription required***)

### COUTINHO RASMI SOKONI

NYOTA wa Brazil, Philippe Coutinho mwenye umri wa miaka 28, atakuwa miongoni mwa wachezaji 10 walioorodheshwa kuuzwa na Barcelona katika dirisha la usajili la mwisho wa msimu huu. (***Star***)

### GOSENS AGEUKA LULU

BARCELONA na Manchester City ni miongoni mwa klabu zinazomtaka kiungo wa kati wa klabu ya Atalanta, Robin Gosens mwenye umri wa miaka 26. (***Sport***)

### UNITED KUMSAJILI HEATON

MANCHESTER United wamekubali kusaini mkataba na mlinda mlango wa Aston Villa, Tom Heaton mwenye umri wa miaka 35. (***Express***)

### ZAHA MAMBO SAFI

TOTTENHAM Hotspur na Everton zinataka kumsajili mshambuliaji wa Crystal Palace na Ivory Coast, Wilfried Zaha mwenye umri wa miaka 28, kwa pauni milioni 40. (***Goal***)

### KRAL ATAKIWA WEST

KLABU ya West Ham inamtaka kiungo wa klabu ya Spartak Moscow na Jamhuri ya Czech, Alex Kral mwenye umri wa miaka 23. (***Sky Sports***)

### WILLIAN AITAMANI CHELSEA

KIUNGO wa Arsenal, Willian mwenye umri wa miaka 32, anataka kurejea katika kikosi cha Chelsea - ikiwa ni chini ya miezi 12 baada ya kuihama klabu hiyo aliyokaa nayo kwa miaka saba. (***Sky Sports***)

### TORRES ASITISHA UVUMI

MLINZI wa Villarreal, Pau Torres (24), amekataa kujadili kuhusu tetesi zinazomhusisha za kuhamia Manchester United msimu huu, kabla ya mchezo wa jana Jumatano wa fainali ya Ligi ya Europa dhidi ya vigogo hao wa jiji la Manchester. (***Metro***)

### ARSENAL, VILLA VITANI

ARSENAL na Aston Villa wataendelea na mipango yao ya kufukuzia saini ya kiungo wa Norwich City, Emiliano Buendia, mwenye umri wa miaka 24. (***Telegraph - subscription required***)

### HUDSON-ODOI KUUZWA

CHELSEA huenda wanataka kumuuza kiungo wao wa kati, Callum Hudson-Odoi (20), huku akitarajiwa kwenda Borussia Dortmund. Dortmund pia wanaweza kuangalia uwezekano wa kumnunua mshambuliaji wa Leeds United, Raphinha mwenye umri wa miaka 24. (***Eurosport***)

## HABARI MICHEZO

# MWAKINYO KUMKARIBISHA RAIS SAMIA KWA UBINGWA

**Na Mwandishi Wetu**

BONDIA Hassan Mwakinyo ameahidi kumpa kipigo kikali mpinzani wake, Antonio Mayala kutoka Angola ikiwa ni asante kwa Rais wa kwanza mwanamke wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

Mwakinyo ambaye atawania mkanda wa Afrika (ABU) wa uzito wa Super Welter atapanda ulingoni kesho kwenye Ukumbi wa Next Door Arena, Masaki katika pambano lililoandaliwa na Kampuni ya Jackson Group Sports.

Bondia huyo alisema amejiandaa vyema na kwa sababu atakuwa anapigana kwa mara ya kwanza tangu Rais Samia aingie madarakani, hatofanya makosa katika pambano hilo lililodhaminiwa na KCB Bank, Plus TV, Multichoice Tanzania, Tanzania Tourism Board, Onomo Hotel, Precision Air, Prestine Logistics, Urban Soul na Global Boxing Stars na Epic Sports Entertainment.

"Nitakuwa napigana kwa mara ya kwanza chini ya utawala wa Rais Mama Samia Suluhu Hassan. Sitamwangusha Rais na Watanzania kwa ujumla, nawaomba mashabiki kufika kwa wingi ili kunipa sapoti," alisema Mwakinyo.

Naye mpinzani wake, Mayala alisema pamoja na kupata taarifa za muda mfupi, amejiandaa vyema ili kuonyesha ubora wake kwamba yeye ni bondia wa ngumi za kulipwa.

> **"Nimekuja kwa ajili ya kushinda na si kupoteza, nilikuwa nafanya mazoezi kwa sababu ngumi ni kazi yangu na siwezi kuruhusu Mwakinyo kushinda na kuchukua mkanda wa Afrika," alisema Mayala.**

Mkurugenzi wa Kampuni ya Jackson Group Sports, Kelvin Twissa, alisema mbali ya pambano hilo pia bondia, Daniel Matefu atazichapa na Pencho Tsvetkov kutoka Bulgaria huku Leila Yazidu akipigana na Joana Nwamerue, ambaye naye anatoka Bulgaria huku Hamisi Palasungulu atazichapa na Ardi Ndembo wa Congo Brazzaville.

Imani Kawaya ataonyeshana kazi na Chris Thompson wa Afrika Kusini, Shabani Jongo atacheza dhidi ya Mnigeria Olanrewaju Durodora ambao watawania uzito wa juu na nyota mwingine Ibrahim Class atazipiga na Sibusiso Zingange wa Afrika Kusini.

Aliongeza kwa kuwaahidi mashabiki wa mchezo huo kujiandaa kushuhudia mapambano yenye ubora kutoka kwa mabondia waliojiandaa kuonyesha ushindani.




Mabondia na makocha kutoka nje ya nchi wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kuwasili nchini kwa ajili ya kupambana na mabondia Watanzania katika usiku wa Rumble in Dar 2 ulioandaliwa na Kampuni ya Jackson Group Sports, pambano litakalofanyika kesho jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Simba yamwonya wakala wa Kagere

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imemwonya wakala wa straika wao, Meddie Kagere aache kumpangia kazi Kocha Mkuu wa timu hiyo, Didier Gomes na badala yake ajikite katika majukumu yake ya kuwatafutia wachezaji klabu.

Simba imelazimika kutoa tamko hilo, siku moja tu baada ya wakala wa Kagere, Patrick Gakumba kusikika kwenye baadhi ya vyombo vya habari akimshutumu Gomes kumweka nje straika huyo katika mechi ya marudiano ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Kaizer Chiefs.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara amesema wakala huyo amemkosea heshima kocha wao, kwa sababu kazi ya kupanga kikosi ni yake na si ya mtu mwingine yoyote.

"Nimesikia kauli hizo za wakala wa Kagere akimlaumu kocha wetu. Hiyo siyo kazi ya wakala. Anamkosea heshima sana kocha wetu. Kwanza inabidi afahamu Simba ilifanya mabadiliko ya lazima ya wachezaji wawili, Joash Onyango na Thadeo Lwanga, ...ile ilivuruga mipango yote ya kocha aliyoipanga mwanzo, inawezekana kabisa angecheza," alisema Manara.

Alisema kuwa siku zote wakala kazi yake ni kuzungumzia na kusimamia maslahi ya mchezaji na si kumpangia kocha mchezaji gani wa kucheza na yupi wa kukaa benchi.

"Sasa tukiruhusu kila wakala atake mchezaji wake acheze itakuwa ni klabu ya aina gani? Tunamheshimu wakala kwa sababu ametuletea mchezaji mzuri, lakini kwa hili ametukosea. Sisi wenyewe hatumpangii kocha itakuwa yeye," aliongeza Manara.

## Prisons yaifuata Namungo mapema

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha inapata matokeo mazuri, kikosi cha Tanzania Prisons kimewasili mapema mkoani Lindi ili kuwavaa wenyeji Namungo FC katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa Juni 2, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa, imeelezwa.

Kocha Msaidizi wa Tanzania Prisons, Shabani Kazumba, aliliambia gazeti hili lengo la kwenda mapema Lindi ni kuendelea 'kuwawasoma' wapinzani wao na hatimaye kutimiza mikakati ya kuondoka na pointi zote tatu katika mchezo huo.

Kazumba alisema kwa uamuzi wao wa kuwahi mkoani humo, watapata fursa ya fursa ya kuzishuhudia mechi mbili za wapinzani wao na kujipanga kuufanyia kazi ubora na mapungufu watakayoyabaini.

Alisema wamejipanga vizuri katika mechi zao tano zilizosalia za msimu huu na wanaamini watapata matokeo chanya kutokana na mikakati waliyojiwekea.

"Hii ligi ni ngumu na sasa iko katika hatua za kufikia ukingoni, tunahitaji kufanya vizuri katika mechi zetu zote zilizosalia, ndio sababu ya kuwahi ili kupata nafasi ya kuwaona wapinzani wetu na kufanyia kazi kile tutakachokiona katika mechi zao mbili kabla hatujakutana nao hapo Juni 2," alisema Kazumba.

Kabla ya kucheza na Tanzania Prisons, wenyeji hao wa Kusini jana waliikaribisha Gwambina na keshokutwa watavaana na mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba kutoka jijini Dar es Salaam.

## JKU yapambana isishuke daraja

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BENCHI la Ufundi la JKU limesema kikosi hicho kinaendelea kujiimarisha ili kuhakikisha malengo ya kubakia katika Ligi Kuu Zanzibar yanatimia.

JKU imekuwa na matokeo yasiyoridhisha katika msimu huu wa 2020/21 ambao unaelekea ukingoni, hali ambayo imewaweka kwenye nafasi isiyo salama.

Ili iweze kujihakikishia inabakia kwenye Ligi Kuu Zanzibar, JKU inatakiwa kushinda michezo yake mitatu iliyobakia.

Kocha Mkuu wa JKU, Omar Khamis "Matu" aliliambia gazeti hili mchezo wake dhidi ya Black Sailor utakaochezwa leo ndio utampa mwanga wa kuendelea kuwa na matumaini ya kusalia kwenye ligi hiyo inayoshirikisha timu 12.

Matu alisema anafahamu mechi hiyo haitakuwa rahisi kwa sababu kila timu inahitaji kupata alama tatu ili kujinusuru na janga la kushuka daraja.

"Nimeendelea kukinoa kikosi changu baada ya kumaliza mechi iliyopita dhidi ya Polisi ambao tulishinda mabao 2-1," alisema Matu ambaye timu yake ipo katika nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na pointi 21.

Michezo
Alhamisi Mei 27, 2021
Nipashe



TOTTENHAM YAFIKIRIA KUMREJESHA POCHETTINO

HABARI UK 22

# YANGA YAJIGAMBA KITAELEWEKA

●●● Yafunguka itakomaa mpaka dakika ya mwisho, Azam FC yatakata FA...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya timu yao kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA, Kocha wa Makipa wa Yanga, Razack Siwa, amesema wataendelea kupambana hadi dakika ya mwisho katika mashindano hayo na hatimaye kutimiza ndoto yao ya kupata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa kwa msimu ujao.

Yanga imetoa kauli hiyo baada ya kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Mwadui FC na sasa itakutana na Biashara United katika hatua inayofuata.

Akizungumza na gazeti hili, Siwa alisema wao wataendelea kujiimarisha ili kupata matokeo bora na kamwe hawatajali au kuangalia matokeo ya timu nyingine.

Siwa ambaye ni raia wa Kenya, alisema wamefurahishwa na ushindi na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wao kwa sababu wamefikia malengo yaliyokusudiwa.

"Tumecheza vizuri na kupata ushindi. Ushindi ni ushindi tu, uwe wa goli moja, mawili ni ushindi na kwa haya tunayoyapata sasa matumaini yapo. Tutapambana hadi dakika ya mwisho bila kuangalia timu nyingine inafanya nini. Sisi tunaendelea na mapambano na mwisho wa michezo ndipo kila kitu kitaamua," alisema Siwa.

Aliongeza mechi zote zilizobakia za Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano hiyo ambayo bingwa wake ataiwakilisha nchi katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika, hivyo wataendelea kujiimarisha zaidi.

Naye Kocha wa Mwadui FC, Salhina Mjengwa, alisema timu yake ambayo msimu ujao itashiriki Ligi Daraja la Kwanza imepoteza mechi hiyo kutokana na makosa binafsi yaliyofanywa na baadhi ya wachezaji wake.

Mjengwa alisema kuna baadhi ya vitu ambavyo wachezaji wake walifanya havikuwa na ulazima walitaka kuvizidisha, ndiyo maana wamepoteza mechi hiyo.

"Goli la kwanza lilikuwa kosa la golikipa na hata goli la pili haikuwa na sababu yoyote ya mchezaji kutaka kupiga chenga pale, kapokonywa ikapigwa ndefu tukafungwa," alisema mchezaji huyo wa zamani wa Mtibwa Sugar ya mkoani Morogoro.

Aliwapongeza Yanga kwa kutumia makosa ya wachezaji wake na kupata ushindi uliowapeleka hatua inayofuata na kuongeza kwa sasa wanakwenda kujipanga upya kwa ajili ya kushiriki na Ligi Daraja la Kwanza.

"Tumeshuka daraja, tumetolewa katika robo fainali, sasa tunakwenda kufanya maandalizi ya kushiriki Ligi Daraja la Kwanza," alisema Mjengwa.

Simba ndio mabingwa watetezi wa mashindano hayo na jana usiku ilishuka dimbani kuvaana na Dodoma Jiji FC kutoka Dodoma katika mechi ya robo fainali ya mwisho iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Wakati huo huo Azam FC imefanikiwa kusonga mbele katika michuano hiyo baada ya kuifunga Rhino Rangers mabao 3-1 katika mechi ya robo fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kambarage mkoani Shinyanga jana.

Mabao ya Azam katika mchezo huo yalifungwa na Ayoub Lyanga, Aggrey Morris na Obrey Chirwa.

Azam sasa itacheza hatua ya nusu fainali dhidi ya mshindi katika mechi kati ya Simba na Dodoma Jiji.




Kiungo wa Azam FC, Mudathir Yahya (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya mchezaji wa Rhino Rangers katika mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kambarage mkoani Shinyanga jana. Azam ilishinda mabao 3-1. **PICHA: MTANDAO**

## SIMBA: MOTO WETU NI ULE ULE

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kikosi chao kutolewa katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, nahodha wa Simba, John Bocco amesema wataendelea na kasi yao kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyobakia na michuano ya FA.

Bocco ambaye alifunga mabao mawili katika ushindi wa magoli 3-0 dhidi ya Kaizer Chiefs alisema wataendelea kujituma kwenye kila mchezo kwa sababu wanahitaji kutimiza malengo ya kutetea mataji yote mawili wanayoyashikilia.

Mshambuliaji huyo alisema wanafahamu mechi zilizosalia ni ngumu kutokana na kila timu kusaka matokeo chanya na hatimaye kufikia malengo.

"Bado hajutamaliza msimu, tutaendelea na mapambano katika mechi zetu zote zilizosalia, tunahitaji kutetea ubingwa wa Ligi Kuu na sisi pia ndio tunashikilia Kombe la FA, nafasi iko wazi, hatutakiwi kupoteza mchezo," alisema mshambuliaji huyo.

Aliongeza kila mchezaji wa Simba anatamani kuona tunamaliza msimu kwa mafanikio na kuwafuta machozi mashabiki wetu baada ya kuondolewa katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**Baada ya mechi ya jana usiku ya Kombe la FA dhidi ya Dodoma Jiji FC, kikosi cha Simba kitajiandaa na safari ya kuelekea Lindi kuwafuata Namungo FC kwa ajili ya mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Majaliwa.**

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042